Toleo la 238 I Septemba 2025

Jarida Maalum la

# NCHI YETU

*Tanzania Imara, Kazi Iendelee*



RAIS SAMIA

# AMEWASIKIA AMEWAFIKIA

Scan kusoma jarida kidijitali

Haliuzwi

Maelezo

# NCHI YETU




Tembelea Tovuti yetu kupata Nakala yako
ya Jarida Maalum la NCHI YETU / **www.maelezo.go.tz**
au Skani QR CODE kupata nakala yako.

# TAHARIRI

## WANANCHI WANAHITAJI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO



Tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani mwezi Machi mwaka 2021, kumekuwa na mageuzi makubwa yanayoendelea kufanyika katika kuhakikisha Watanzania wanapata maendeleo.

Mageuzi haya yamegusa sekta zote za kiuchumi na kijamii zikiwemo za ujenzi wa miundombinu ya barabara; viwanja vya ndege; hospitali zikiwemo zile za kanda, zahanati na vituo vya afya; miradi ya maji; ujenzi wa shule; reli ya kisasa ya SGR, Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo pamoja na ununuzi wa ndege na meli za kisasa.

Miradi yote hii ya maendeleo imekuwa na mchango mkubwa katika ustawi wa Watanzania ambao wamekuwa wakitumia fursa zinazotokana na utekelezaji wa miradi hii. Hata hivyo, ili Watanzania waweze kutumia fursa mbalimbali za utekelezaji wa Serikali kwenye miradi ya maendeleo ni lazima awe na taarifa sahihi kuhusu miradi hiyo.

Kwa kuona hilo, Idara ya Habari - MAELEZO iliyo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, iliona umuhimu wa kutangaza utekelezaji wa Serikali kwenye miradi ya maendeleo katika ngazi ya mikoa na halmashauri kupitia program maalumu ya **TUMEWASIKIA, TUMEWAFIKIA,** ambayo ilihusisha uchukuaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye halmashauri na mikoa na kuitangaza kupitia vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kufanya mikutano ya Wakuu wa Mikoa kuelezea mafanikio ya utekelezaji huo.

Mikoa iliyoshiriki awamu ya kwanza ya program ya kutangaza utekelezaji huo kwa mwaka 2025/2026 ni Katavi, Tabora, Kigoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Geita, Kagera, Simiyu, Mara, Arusha na Tanga ambapo Wakuu wa Mikoa walizungumza na Waandishi wa Habari kuelezea utekelezaji wa mikoa wakiwa mubashara katika vyombo vya habari vikiwemo; televisheni, redio na mitandao ya kijamii.

Kwa muktadha huo huo wa kuendelea kutangaza mafanikio ya utekelezaji wa Serikali kwenye miradi ya maendeleo ili kuwasaidia Watanzania kutumia fursa za uwepo wa miradi hiyo, Idara ya Habari imeandaa Jarida hili Maalum la **NCHI YETU** ambalo limesheheni makala na habari maalum za miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Serikali katika mikoa 12 iliyofikiwa.

Ni imani yetu kuwa, mikoa mingine pamoja na wizara na taasisi mbalimbali za Serikali zinashiriki kikamilifu katika kutangaza mafanikio ya utekelezaji wa Serikali ili wananchi wapate taarifa za kutosha na kutumia taarifa hizo kama fursa kwa manufaa yao ya kiuchumi na kijamii.

**Gerson Msigwa**
Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali


## BODI YA WAHARIRI

**Mwenyekiti**
Gerson Msigwa
Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali

**Wajumbe**
Rodney Thadeus
Zamaradi Kawawa
Aron Msigwa

**Msanifu**
Kiamba H. Magogo

**Mchapaji**
Tony Richie Printing



**Idara ya Habari MAELEZO**

S.L.P 25
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 2322129
Barua pepe: maelezo@michezo.go.tz
www.maelezo.go.tz










# Ndani ya Jarida


01 Dira ya 2050: Ahadi mpya, Tanzania Mpya

04 Trilioni 56.49 Zapitishwa Bungeni Kuimarisha Ukuaji Uchumi

07 Waandishi Wakumbushwa Uzalendo na Maadili Kuelekea Uchaguzi Mkuu 2025

10 Rais Samia Aboresha Mazingira ya Kazi na Maslahi kwa Watumishi wa Umma

13 Tanzania Yaunganishwa kila Kona Kuwezesha Uchumi Mpya

18 Sekta ya Madini Injini ya Uchumi Inayochanua

24 Awamu ya Sita Yaweka Mazingira Mazuri ya Uendelezaji Viwanda, Biashara

30 Samia Ajenga Shule 26 za Sayansi kwa Wasichana

34 Shilingi Trilioni 5.6 Zatumika Kuifungua Mwanza Kiuchumi

37 Uimara wa JWTZ Wawezesha Tanzania Kuwa Kisiwa cha Amani

40 Shilingi Trilioni 1.34 Zachochea Ustawi wa Wananchi Katavi

45 Trilioni 11.4 Zawasha Moto wa Maendeleo Kigoma

















**49** | Shinyanga Yang’ara Miaka Minne ya Rais Samia

**52** | Simiyu Inavyofunguka kwa Uwekezaji wa Serikali

**56** | Arusha Yapaa Kiuchumi, Pato la Wananchi Laongezeka

**61** | Mara Wanufaika na Uwekezaji Uliofanywa na Serikali

**66** | Miaka minne ya Rais Samia Singida Yashuhudia Maendeleo Makubwa

**69** | Miradi Mikubwa ya Kilimo na Maendeleo Yaboresha Maisha

**75** | Jinsi Shilingi Trilioni 1.131 Zilivyochagiza Maendeleo Kagera

**79** | Katiba na Sheria Waeleza Mafanikio ya Maelekezo ya Dkt. Samia

**82** | Geita Yajivunia Samia Kukamilisha Miradi Lukuki

**88** | Miradi Inayotekelezwa na Serikali Yaboresha Maisha Tanga

**94** | Rais Samia: Nguvu ya Michezo Kuunganisha Watanzani

**99** | Alphonce Simbu Atwaa Medali ya Dhahabu Mashindano ya Riadha Duniani 2025




# Dira ya 2050: Ahadi Mpya, Tanzania Mpya

- Amani na Utulivu ndio Msingi wa Maendeleo - Samia

Na **Aron Msigwa - MAELEZO**

> Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kwa utajiri wa mali asili, ardhi na jiografia, niliyoiita Lulu ya pekee katika historia ya Afrika."

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Ni kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Maneno haya yalisikika tena hivi karibuni, yakirejewa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050.

Rais Samia aliitumia kauli hii ya Mwalimu Nyerere, kama msingi thabiti wa kuwakumbusha Watanzania juu ya utajiri huu wa rasilimali na haja ya kuutumia kuondoa changamoto za kiuchumi zinazokabili taifa.

Rais Samia katika uzinduzi wa dira hiyo alisisitiza kuwa jukumu la viongozi na wananchi wote ni kubuni na kutekeleza mipango madhubuti ya kuutumia utajiri huu ili kufaidisha maisha ya kila Mtanzania.

"Tunayo mifano mingi ya nchi zilizokuwa maskini kwa rasilimali lakini sasa watu wake wana ustawi mkubwa kutokana na mipango na mikakati waliyojiwekea," alisema Rais Samia, akiongeza kuwa dhamira ya serikali yake ni kuhakikisha faida zitokanazo na utajiri wa nchi zinawafikia wananchi wote.

# Misingi Mikuu ya Dira ya 2050

Dira ya 2050 inajengwa juu ya misingi mikuu minne inayolenga kuleta mabadiliko ya kweli kwa taifa. Msingi wa kwanza ni Utawala Bora, Amani, Usalama na Utulivu. Rais Samia alikumbusha kwamba Tanzania imedumisha historia ya kupokezana madaraka kwa amani, na kwamba utulivu huu ndio msingi wa maendeleo.

Msingi wa pili ni Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani. Dira hii inalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu kwa kuimarisha uwezo wa kifedha, kuchochea vyanzo bunifu vya ufadhili na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Msingi wa tatu unazingatia kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii. Lengo ni kujenga rasilimali watu yenye ujuzi, maisha yenye staha, usawa na utu kwa Watanzania. Hili litafikiwa kupitia malezi bora ya watoto, elimu bora, huduma bora za afya kwa wote, nishati safi na mifumo imara ya hifadhi ya jamii.

Dira inasisitiza umuhimu wa kujenga jamii jumuishi inayozingatia usawa wa kijinsia, mshikamano wa kitaifa na kupunguza tofauti za maendeleo kati ya mikoa na makundi ya kijamii.

Msingi wa mwisho ni Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi. Dira inalenga kuifanya Tanzania kuwa kinara wa kimataifa katika uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali asili, huku ikijenga uwezo wa taifa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Dira ya 2050 inajengwa juu ya misingi mikuu minne inayolenga kuleta mabadiliko ya kweli kwa taifa. Msingi wa kwanza ni Utawala Bora, Amani, Usalama na Utulivu. Rais Samia alikumbusha kwamba Tanzania imedumisha historia ya kupokezana madaraka kwa amani, na kwamba utulivu huu ndio msingi wa maendeleo.

Msingi wa pili ni Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani. Dira hii inalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu kwa kuimarisha uwezo wa kifedha, kuchochea vyanzo bunifu vya ufadhili na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Msingi wa tatu unazingatia kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii. Lengo ni kujenga rasilimali watu yenye ujuzi, maisha yenye staha, usawa na utu kwa Watanzania. Hili litafikiwa kupitia malezi bora ya watoto, elimu bora, huduma bora za afya kwa wote, nishati safi na mifumo imara ya hifadhi ya jamii.

Dira inasisitiza umuhimu wa kujenga jamii jumuishi inayozingatia usawa wa kijinsia, mshikamano wa kitaifa na kupunguza tofauti za maendeleo kati ya mikoa na makundi ya kijamii.

Msingi wa mwisho ni Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi. Dira inalenga kuifanya Tanzania kuwa kinara wa kimataifa katika uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali asili, huku ikijenga uwezo wa taifa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

# Sekta Tisa za Kimkakati na Malengo ya Dira 2050

Ili kufikia malengo haya makubwa, Dira ya 2050 imebainisha sekta tisa za kimageuzi zilizopewa kipaumbele, ikiwemo kilimo, utalii, viwanda, ujenzi, madini, uchumi wa buluu, michezo na ubunifu, huduma za kifedha, na sekta ya huduma. Sekta hizi zinalenga kujenga uwezo wa nchi kuzalisha ajira nyingi, kuongeza mauzo nje, kuchochea ukuaji wa sekta zingine, na kuongeza mapato ya Serikali.



# Misingi Mikuu ya Dira ya 2050

Uchumi: Kuwa na Pato la Taifa la Dola za Marekani Trilioni 1 na Pato la Mtu Mmoja la Dola za Marekani 7,000. Hili linamaanisha wastani wa kipato cha shilingi 1.52 milioni kwa mwezi kwa kila Mtanzania ifikapo 2050.

Maisha Bora: Kutokomeza umaskini uliokithiri na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkuu wa chakula Afrika na kuwa miongoni mwa nchi 10 bora duniani. Pia, Mtanzania ataishi wastani wa miaka 75 yenye afya na furaha.

Elimu na Afya: Kutokomeza vifo vya wajawazito na watoto wachanga, kuimarisha huduma bora za afya kwa wote, na kuhakikisha watanzania wote wanapata elimu bora yenye ujuzi wa kidijitali.

Mazingira na Teknolojia: Kuifanya Tanzania kuwa kinara wa mazingira duniani na kuongeza matumizi ya umeme kwa kila mtu hadi kilowati 3000 kwa mwaka. Huduma za Serikali zitatolewa kwa njia ya kidijitali kwa zaidi ya asilimia 80.

• Usawa: Kupunguza pengo la kijinsia kwa angalau asilimia 85.

Rais Samia anasema: "Maudhui ya Dira 2050 yametokana na maoni na matakwa ya Watanzania wenyewe. Tumefikiri wenyewe, tumeandika wenyewe, tumepanga wenyewe, na tutatekeleza wenyewe."

Alisisitiza kuwa safari hii ni ndefu, lakini kwa umoja na bidii ya Watanzania, Dira hii ya maendeleo itafikiwa.

# Ushirikishwaji na Hatua Zilizochukuliwa

Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango, Dkt. Fred Msemwa, alieleza kuwa mchakato wa kuandaa Dira hii ulikuwa shirikishi.

"Tumetumia njia mbalimbali kuhakikisha kila Mtanzania popote alipo anatoa maoni," alisema Dkt. Msemwa, akibainisha kuwa zaidi ya watanzania milioni 1.1 walitoa maoni yao ana kwa ana na wengine kupitia simu na mitandao ya kijamii. Ushiriki wa vijana, hasa, ulikuwa mkubwa, ukiakisi demografia ya taifa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mhe. Prof. Kitila Mkumbo, alibainisha kuwa maoni ya viongozi wa kitaifa, waliopo madarakani na waliostaafu, yalikusanywa ili kuhakikisha kuna mwendelezo mzuri wa kihistoria. Viongozi 19 wa vyama vya siasa vilivyosajiliwa pia walishirikishwa na kutoa maoni yao.

Rais Samia anasema: "Maudhui ya Dira 2050 yametokana na





# Trilioni 56.49 Zapitishwa Bungeni Kuimarisha Ukuaji Uchumi

- Kima cha Chini cha Mshahara Kimeongezeka
- Pensheni ya kila Mwezi kwa Wastaafu Imeongezeka

Na **Aron Msigwa - MAELEZO**

Mnamo Juni 24, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliweka historia kwa kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26 yenye thamani ya Shilingi trilioni 56.49.

Bajeti hii ilipitishwa kwa kishindo, huku asilimia 98.7 ya wabunge wakipiga kura ya ndiyo, ikiashiria imani kubwa kwa serikali katika malengo yaliyokusudiwa na bajeti hiyo.

Akiwasilisha bajeti hiyo mjini Dodoma, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, alisisitiza kuwa imeandaliwa kwa kuzingatia malengo ya kufikia ukuaji imara wa uchumi.
Alisema kuwa bajeti hiyo inalenga kuimarisha miradi ya uzalishaji, kuboresha rasilimali watu hususan katika sekta za huduma za jamii, na kuchochea uchumi shindani na shirikishi.

“Kupitia bajeti hii, serikali inatarajia kuimarisha uzalishaji viwandani, kukuza uwekezaji, biashara, na kuchochea maendeleo ya watu ili kufikia

## Vipaumbele vya Bajeti

Katika juhudi za kuimarisha uchumi, serikali imetenga vipaumbele kadhaa. Kwanza, inaendeleza juhudi za kudhibiti mfumuko wa bei kwa kuimarisha sekta za uzalishaji, kuongeza matumizi ya gesi asilia inayozalishwa nchini, na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza utegemezi wa mafuta ya petroli kutoka nje.

Aidha, bajeti hiyo imelenga kuboresha mazingira ya uzalishaji wa mbolea, mafuta ya kula, sukari na bidhaa nyingine muhimu ili kupunguza uagizaji wake kutoka nje ya nchi. Serikali pia imesema itaendelea kutekeleza sera madhubuti za fedha na kuongeza uzalishaji wa mazao ili kuwezesha upatikanaji wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani.

Kwa kutambua umuhimu wa sekta za uzalishaji katika kukuza Pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi, serikali imetenga kiasi cha Shilingi trilioni 10.24 kwa ajili ya sekta hizo, sawa na asilimia 18.12 ya bajeti yote ya Serikali ya mwaka 2025/26.

Bajeti pia imezingatia maandalizi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo, na pia imetoa kipaumbele kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambao utagharamiwa na fedha za ndani.

Sekta ya kilimo nayo imetengewa kiasi cha Shilingi trilioni 1.9, ikiwa ni ongezeko la asilimia 203.6 kutoka bajeti ya mwaka 2021/22.

## Uwekezaji Miundombinu na Huduma za Jamii

Serikali inaendelea kugharamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo. Kwa upande wa miundombinu, Shilingi trilioni 1.58 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege.

Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli, ikiwemo mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), umepatiwa Shilingi trilioni 1.68. Zaidi ya hayo, Shilingi bilioni 574.8 zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) na mradi wa kusambaza umeme vijijini kupitia REA.

Kwa maandalizi ya AFCON 2027, Aidha Shilingi bilioni 179.8 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa viwanja.

Katika sekta ya elimu, serikali imeendelea kuboresha mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati kwa kuwekeza Shilingi bilioni 636.0, na Programu ya Elimu Msingi na Sekondari bila Ada imetengewa Shilingi bilioni 444.7.

Miradi ya maji mijini na vijijini imetengewa Shilingi bilioni 378.7. Huduma za afya nazo zimepewa kipaumbele, huku Shilingi bilioni 414.7 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba, Shilingi bilioni 47.2 kwa ujenzi wa hospitali, na Shilingi bilioni 7.3 kwa ajili ya vituo vya afya na zahanati.

## Mishahara, Pensheni, na Ulipaji wa Madeni

Kwa kutambua mchango wa watumishi wa umma, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliongeza kima cha chini cha mshahara kutoka Shilingi 370,000 hadi Shilingi 500,000, sawa na ongezeko la asilimia 35.1.

Aidha, kwa ajili ya wastaafu, serikali imeongeza kima cha chini cha pensheni ya kila mwezi kwa wanaolipwa na Hazina kutoka Shilingi 100,125.9 hadi Shilingi 250,125.9, sawa na ongezeko la asilimia 149.8.

Serikali inaendelea kusimamia mifuko ya hifadhi za jamii ili kuhakikisha inabaki himilivu. Tangu mwaka 2021 hadi Mei 2025, Serikali imelipa madeni yenye thamani ya Shilingi trilioni 2.67, huku ikiwa imeandaa utaratibu wa kumaliza deni lote la "Pre-99" ndani ya miaka mitatu.

Aidha, bajeti hiyo imepunguza ushuru wa forodha kwa mashine za kielektroniki za kukusanya mapato (EFD), kadi za vitambulisho vya Taifa zinazoingizwa na NIDA, na vitenge ili kuweka unafuu kwa wananchi na wafanyabiashara.

Serikali imesema kwamba hatua hizi zote zinalenga kuimarisha uchumi, kuvutia uwekezaji, kuongeza ajira na kukuza maendeleo ya kweli nchini.

## Kupunguza Kodi, Kukuza Viwanda na Biashara

Bajeti ya mwaka 2025/26 imetoa unafuu wa kodi katika maeneo mbalimbali ili kuchochea uzalishaji wa ndani. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na malighafi, vipuri na mashine zinazotumika kutengeneza viatu vya ngozi na nguo; vifungashio vya maziwa na kahawa; malighafi za kutengeneza sabuni, mabomba ya plastiki na nyaya za umeme.






# Waandishi Wakumbushwa Uzalendo na Maadili Kuelekea Uchaguzi Mkuu 2025

Na **Naishooki Makeseni, MAELEZO**

Wakati Tanzania inaelekea katika kipindi muhimu cha Uchaguzi Mkuu wa 2025, kwa kutambua umuhimu wa habari katika mchakato huu, Julai 9, serikali iliandaa kongamano la kipekee lililokutanisha wadau mbalimbali. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Idara ya Habari - MAELEZO, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), waliratibu kongamano lililowaleta pamoja wadau wa habari na Jeshi la Polisi, ikiwemo Jeshi la Polisi. Lengo kuu la kongamano hilo lilikuwa kukumbushana misingi ya maadili, uzalendo, na umakini wa kitaaluma katika kuripoti habari kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

## Alichosema Dkt. Biteko kuhusu Maadili

Katika hotuba yake ya uzinduzi Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko aliwasifu wadau wa habari kwa mchango wao, akisisitiza umuhimu wao katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Alikumbusha jinsi serikali ya sasa ilivyofungua vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa, ikionesha nia yake ya dhati ya kuheshimu uhuru wa habari.

"Majuma mawili ya mwanzo tangu Serikali ya awamu ya sita ilipoingia madarakani ilianzisha hatua ya kufufua vyombo vilivyokuwa vimefungiwa," alisema Dk Biteko na kuendelea kuwaasa waandishi wa habari kuiishi misingi ya taaluma yao na kuepuka habari za kichochezi au zenye nia ovu.

Hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, ililifanya kongamano hilo kuwa darasa rasmi.

Prof. Kabudi, ambaye pia ni mwana habari mbobevu, aliwaeleza wanahabari umuhimu wa uzalendo, huku

akiwasisitiza kuripoti taarifa sahihi na zisizo na upendeleo. Alisisitiza kuwa wakati wa uchaguzi, uhitaji wa taarifa sahihi huongezeka na ni jukumu la wanahabari kutoa ukweli bila kupotosha.

Katika hotuba yake ya uzinduzi Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko aliwasifu wadau wa habari kwa mchango wao, akisisitiza umuhimu wao katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Alikumbusha jinsi serikali ya sasa ilivyofungua vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa, ikionesha nia yake ya dhati ya kuheshimu uhuru wa habari.

“Majuma mawili ya mwanzo tangu Serikali ya awamu ya sita ilipoingia madarakani ilianzisha hatua ya kufufua vyombo vilivyokuwa vimefungiwa,” alisema Dk Biteko na kuendelea kuwaasa waandishi wa habari kuiishi misingi ya taaluma yao na kuepuka habari za kichochezi au zenye nia ovu.

Hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, ililifanya kongamano hilo kuwa darasa rasmi.

Prof. Kabudi, ambaye pia ni mwana habari mbobevu, aliwaeleza wanahabari umuhimu wa uzalendo, huku akiwasisitiza kuripoti taarifa sahihi na zisizo na upendeleo. Alisisitiza kuwa wakati wa uchaguzi, uhitaji wa taarifa sahihi huongezeka na ni jukumu la wanahabari kutoa ukweli bila kupotosha.

## Kauli za wadau

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Bw. Deodatus Balile, alipongeza Wizara ya Habari kwa kuandaa kongamano hilo, akisisitiza kuwa si jambo dogo kuwakusanya wadau wote hao muhimu katika sehemu moja.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Bw. Kenneth Simbaya, alisisitiza msimamo wake wa kuunga mkono michakato ya kidemokrasia na kutoa taarifa sahihi. "Tunataka kuliunganisha Taifa na si kuwa sehemu ya mipasuko". alisisitiza Bw. Simbaya

Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), David Misime, alithibitisha kwamba Jeshi la Polisi lina jukumu la kulinda usalama wa waandishi wa habari kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Aliwahimiza wanahabari kuripoti habari zinazojenga taswira chanya ya taifa, huku akihimiza uwajibikaji.

“Wengine wamezoea kuandika habari mbaya lakini pia kuna mazuri mengi ambayo yangeweza kuandikwa lakini wajibu wetu wa pamoja ni kukumbushana kujitambua na kujitawala kama watanzania, nchi yetu wote ni na hatuna nchi nyingine lazima tujitambue tofauti na wengine” alisema DCP Misime.

Kauli yake iliungwa mkono na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, SACP Benjamin Kuzaga, aliyepongeza serikali kwa kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB), akieleza kuwa inasaidia kudhibiti waandishi wasio na taaluma na maadili.

## Ahadi za Serikali

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Bw. Gerson Msigwa, akihitimisha kongamano hilo alieleza matarajio na ahadi za serikali kwa vyombo vya habari. Alisisitiza kuwa serikali inatarajia wanahabari watafanya kazi zao kwa haki, bila upendeleo, na kujiepusha na habari zinazohamasisha ukabila, au ubaguzi wa aina yoyote.

Pia, aliahidi kuwa serikali itaendelea kuwalinda wanahabari, kuwapa ushirikiano, kutoa mwongozo maalumu wakati wa uchaguzi, na kuboresha mazingira yao ya kazi.

" Tunatarajia vyombo vya habari vitatekeleza majukumu yao kwa haki na kuepuka upendeleo pia tunatarajia waandishi wa habari watahakikisha kuwa wanalında utaifa wa Taifa letu. Tunatarajia watajiepusha na habari zinahamasisha ukabila na ubaguzi wa aina zote" alisisitiza Msigwa.

Kwa kuzingatia matakwa ya wadau na ahadi za serikali, Tanzania inaonekana ipo kwenye njia sahihi kuelekea uchaguzi mkuu wenye amani, uwazi na maendeleo ya kitaifa.



*Wadau wa Habari na Utangazaji wakiwa katika mkutano wa kujadili mchango wa Sekta ya Habari katika kufanikisha Uchaguzi Mkuu 2025 uliofanyika Julai 9, 2025 katika Ukumbi wa Mlimani City.*



*Wadau wa Habari na Utangazaji wakiwa katika mkutano wa kujadili mchango wa Sekta ya Habari katika kufanikisha Uchaguzi Mkuu 2025 uliofanyika Julai 9, 2025 katika Ukumbi wa Mlimani City.*



*Makamanda wa Mikoa, Makamanda wa Vikosi, Maafisa Polisi Jamii na Maafisa Habari wa Jeshi la Polisi wakiwa katika Mkutano wa Kujadili Mchango wa Sekta ya Habari katika kufanikisha Uchaguzi Mkuu 2025 uliofanyika Julai 9, 2025 katika Ukumbi wa Mlimani City.*




# Rais Samia Aboresha Mazingira ya Kazi na Maslahi kwa Watumishi wa Umma

Na **Aron Msigwa - MAELEZO**

> **Ahadi yetu kwenu wafanyakazi ni kwamba tutaendelea kuboresha mazingira ya kazi, yakiwemo maslahi ya wafanyakazi kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu."**
>
> Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Tangu alipoingia madarakani Machi 19, 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameonesha wazi nia yake ya kuboresha mazingira ya kazi na maslahi kwa watumishi wa umma nchini. Ukweli huo unathibitishwa na vitendo na hatua anazochukua.

Katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Singida Mei 1, 2025, Rais Samia alitangaza habari njema kwa watumishi wa umma. Alitangaza ongezeko la asilimia 35.1 kwenye kima cha chini cha mshahara, akieleza kuwa uamuzi huo ulitokana na kuimarika kwa uchumi wa nchi na mchango mkubwa unaofanywa na wafanyakazi.

"Baada ya kuangalia uchumi ulivyopanda, kwa sababu ya nguvu zenu wafanyakazi, nina furaha kuwatangazia kuwa mwaka huu serikali itaongeza kima cha chini cha mshahara kwa watumishi wa umma kwa asilimia 35.1," alisema Rais Samia,

Aidha akihutubia wakati wa kufunga Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 27, 2025, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alieleza kuwa atapandisha kima cha chini

cha mshahara kutoka Shilingi 370,000 hadi Shilingi 500,000. Ongezeko hili la asilimia 35.1 lilianza kutumika rasmi mwezi Julai, na kutoa unafuu mkubwa kwa watumishi wa umma.

Aidha, alisema serikali imetoa ajira katika taasisi mbalimbali za umma kwa watumishi 135,626, na vibali vya ajira mbadala 41,673 vilivyotolewa ili kujaza nafasi zilizobaki wazi kwa sababu mbalimbali.

Pia, alisema katika kutambua mchango wa watumishi wa umma katika maendeleo na ustawi wa Taifa, serikali imechukua hatua mbalimbali kuboresha maslahi yao. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya ushughulikiaji wa maslahi ya watumishi wa umma, kuwajengea uwezo, pamoja na kuwapatia vitendea kazi.

Katika kipindi hiki, jumla ya watumishi wa umma 611,063 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo, 42,557 wamebadilishwa kada, na 9,620 wamefanyiwa mabadiliko ya mshahara binafsi.

Aidha, katika kipindi hiki serikali imeendelea kulipa jumla ya Shilingi bilioni 252.76 za malimbikizo ya mishahara ya watumishi 150,647 , na shilingi bilioni 33.29 za malimbikizo ya mishahara ya wastaafu 10,022.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene anaeleza kuwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake ameboresha maslahi ya watumishi wa umma hatua ambayo imeongeza ufanisi mahala pa kazi.

Mhe. Simbachawene anaeleza kuwa Rais Samia ameboresha maslahi ya watumishi kwa kupunguza kodi ya mapato (PAYE) kutoka 9% hadi asilimia 8% na kuongeza kima cha chini cha mshahara kinachopaswa kukatwa kodi kutoka Shilingi 170,000 hadi Shilingi 270,000 ambapo hatua hii imeifanya serikali isamehe takribani Shilingi bilioni 14.78 kutoka kwa watumishi wa umma.

Mhe. Simbachawene anaendelea kueleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imefanya maboresho katika umri wa watoto wategemezi wa wanachama wa NHIF kwa kuongeza umri wa watoto wategemezi wa wanachama wa mfuko huo kutoka miaka 18 hadi miaka 21 ambapo watoto 65,353 wamenufaika na jumla ya shilingi 3,702,636,040 zimetumika katika kugharamia matibabu yao.





*Wafanyakazi kutoka Wizara mbalimbali, Taasisi za umma na binafsi wakipita mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa Maadhimisho ya sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi ambazo Kitaifa zimefanyika katika uwanja wa Bombadia mkoani Singida tarehe Mei 1, 2025.*

Pia, serikali imefuta tozo ya asilimia 6 iliyokuwa ikitozwa kutoka katika mishahara ya watumishi wa umma walionufaika na mikopo ya elimu ya juu ambapo jumla ya shilingi trilioni 1.1 zimebaki kwa watumishi husika. Pia serikali imeongeza viwango vya posho za kujikimu kwa safari za kikazi ndani ya nchi na posho ya kazi za masaa ya ziada.

“Katika kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa umma Serikali imeongeza mshahara wa kima cha chini na kutoa nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa mwaka 2023/24 na 2024/25 ambayo imekuwa ikitolewa kila mwezi, kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 130,463 yenye jumla ya shilingi bilioni 226.58 ambayo yalipokelewa na kushughulikiwa.

Mhe. Simbachawene ameongeza kuwa serikali imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi ya jumla ya wastaafu 10,022 kutoka kwa waajiri yenye jumla ya shilingi bilioni 33.29 pia imepandisha vyeo jumla ya watumishi wa umma 610,733, kubadilisha kada watumishi 42,515 na kutoa uteuzi kwa watumishi 3,208.

Aidha, katika kuboresha zaidi mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa umma anaeleza kuwa serikali imeunda mfumo wa huduma mtandao kwa watumishi (Watumishi Portal) unaowawezesha watumishi wa umma kupata huduma mbalimbali za kiutumishi moja kwa moja bila kulazimika kwenda kwenye ofisi za waajiri wao.

Aidha, Mhe. Simbachawene anasema jumla ya watumishi 157,512 wamesafishiwa taarifa zao za kiutumishi huku watumishi 10,725 wakibadilishiwa vyeo.

Pia jumla ya watumishi 3,877 wamerekebishiwa majina, watumishi 9,269 wamefanyiwa mabadiliko ya mishahara na watumishi 2,558 wamerejeshwa kwenye utumishi wa umma.

# Tanzania Yaunganishwa Kila Kona Kuwezesha Uchumi Mpya



*Daraja la Ruaha Mkuu lenye urefu wa mita 133 pamoja na Barabara ya Kidatu – Ifakara yenye urefu wa kilomita 66.9 mkoani Morogoro.*

Na **Aron Msigwa – MAELEZO**

Tanzania inashuhudia mabadiliko makubwa katika sekta ya ujenzi, ikileta mageuzi makubwa kwenye miundombinu.

Chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchi inaunganishwa zaidi kuliko wakati wowote ule, kupitia mtandao wa barabara za lami, madaraja imara, vivuko vya kisasa, na viwanja vya ndege vilivyoboreshwa.

Mageuzi haya yanachochea kasi ya uchumi kwa kurahisisha usafiri wa bidhaa na watu kote nchini.

Katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia, mtandao wa barabara unaosimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) umeongezeka kutoka kilometa 36,361.95 hadi kilometa 37,435.04. Sababu ya kuongezeka kwa mtandao huo ni kupandishwa hadhi kwa barabara za wilaya kuwa barabara za kitaifa.

Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega anaeleza kuwa barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 1,365.87 zimejengwa kwa kiwango cha lami zikiwemo za Kasulu - Kabingo (kilometa 184); Mbinga – Mbamba Bay (kilometa 66); Mpemba – Isongole (kilometa 50.3); Lusitu - Mawengi (kilometa 50); Njombe – Moronga Section (kilometa 53.9); Moronga – Makete Section (kilometa 53.5); Rudewa – Kilosa (kilometa 24); Morocco – Mwenge (kilometa 4.3); Makutano – Natta (Sanzate) Section (kilometa 50); Loliondo – Mto wa Mbu (sehemu ya Waso – Sale Jct (kilometa 50).



*Barabara ya Mbinga - Mbamba Bay yenye urefu wa kilometa 66 iliyopo mkoani Ruvuma.*

Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja nane (8) yakiwemo, Daraja la Gerezani (meta 40) Dar es Salaam; Daraja jipya la Tanzanite (kilometa 1.03) Dar es Salaam; Daraja la Wami (meta 510) Pwani; Daraja la Kitengule (meta 140) Kagera; Daraja la Kiyegeya (m 25) Morogoro; Daraja la Ruhuhu (meta 98) Ruvuma; Daraja la Mpwapwa (meta 60) Dodoma na Daraja la Msingi (meta 100) Singida.

Katika hatua nyingine Waziri Ulega anaeleza kuwa ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 2,380.4 unaendelea nchini kote pamoja na ujenzi wa madaraja 12 ambayo yapo katika hatua mbalimbali. Madaraja hayo ni Mbangala (meta 120), Lower Mpiji, Mbambe (meta 81), Simiyu (meta 150), Pangani (meta 525), Sukuma, Kerema Maziwani, Kibakwe, Mirumba na Jangwani.

Kwa upande wa daraja la John Pombe Magufu(li Kigongo – Busisi), Waziri Ulega anaeleza kuwa ujenzi wake umekamilika na tayari linatumiwa na wananchi.

Anaeleza kuwa Serikali imetumia zaidi ya Shilingi bilioni 700 kukamilisha kazi hiyo. Aidha, anasema daraja hilo lililopo kwenye Ziwa Victoria ni refu kuliko yote katika ukanda wa Afrika Mashariki na kati na la sita barani Afrika likiunganisha eneo la Kigongo wilayani Misungwi na eneo la Busisi, Wilaya ya Sengerema.

Kuanza kutumika kwa daraja hilo lenye njia nne pamoja na njia za watembea kwa miguu kila upande kumerahisisha shughuli za usafirishaji katika mikoa ya Geita, Kagera, Mwanza, Kigoma na nchi jirani za Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Wasafiri walikuwa wanatumia muda mrefu kuvuka eneo la Kigongo -Busisi kwa kutumia vivuko.

Pia uwepo wa daraja hilo umerahisisha huduma ya usafiri kwa wagonjwa kutoka mikoa ya Geita, Kigoma na Kagera wanaokimbizwa kwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando.

Kwa upande wa miji na majiji Mhe Ulega anasema serikali imechukua hatua mbalimbali ili kupunguza msongamano wa magari hususani katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dodoma.

Anasema hatua hizo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya barabara eneo la Ubungo, TAZARA, Chang'ombe na Uhasibu. Aidha, mazungumzo na Serikali ya Japan kupitia Shirika Lake la Maendeleo la JICA ya kupata fedha za mkopo nafuu kwa ajili ya ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Mwenge na Morocco yanaendelea.

Pia anaeleza kuwa katika kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya mafuriko katika eneo la Jangwani ambalo limekuwa likisababisha barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani kufungwa na kusababisha adha kubwa kwa watumiaji wa barabara, serikali imefanya usanifu wa daraja jipya lenye urefu wa meta 390, kimo cha meta 14.5 kutoka usawa wa bahari ambao ni wastani wa meta 8.5 juu ya usawa wa barabara, pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa meta 700 ili kukabiliana na changamoto hiyo. Daraja hilo litajengwa kutoka Magomeni kwenye makutano ya Barabara za Kawawa na Morogoro hadi Fire kwenye makutano ya Barabara ya Morogoro na Umoja wa Mataifa (UN)

Mkataba wa ujenzi wa Daraja la Jangwani ulisainiwa kati ya TANROADS na Mkandarasi, M/s China Communications Construction Company Ltd kutoka China Oktoba 22, 2024 kwa gharama ya shilingi bilioni 97.1 na muda wa ujenzi ni miezi 24. Ujenzi wa daraja hilo tayari umeanza.

Kwa upande wa Jiji la Dodoma, serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje (Outer Ring Road) katika jiji la Dodoma kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 112 ambapo sehemu ya kwanza ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Bandari Kavu (kilometa 52.3) ujenzi wake umefikia asilimia 86, na sehemu ya pili ya Ihumwa Bandari Kavu – Matumbulu – Nala (kilometa 60) ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 85.

Pia, serikali imeendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji wa viwanja vya ndege vya Msalato, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na Lake Manyara. Miradi hii ikikamilika viwanja vitarejeshwa TAA kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji.

Katika kuhakikisha usalama na uimara wa muda mrefu wa barabara katika maeneo mbalimbali nchini, serikali imeendelea kujenga na kuboresha mizani ya kupima uzito wa magari ili kulinda barabara zisiharibike mapema na kuimarisha udhibiti wa uzito wa magari.

Katika eneo hili Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS imejenga mizani ya Rubana mkoani Mara na ujenzi wa mizani ya Kemokouwa mkoani Arusha, ujenzi wa mizani ya Igagala mkoani Njombe na Kizengi mkoani Tabora unaendelea.

Aidha, Waziri Ulega anaeleza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo ya kuwepo kwa taa za barabarani kama mojawapo ya njia za kupunguza ajali na kuokoa maisha ya watu hapa nchini. Kama sehemu ya utelekezaji wa maelekezo hayo, jumla ya taa za barabarani 4,680



*Barabara ya kiwango Cha lami kutoka Sumbawanga - Matai - Kasanga yenye urefu wa kilomitakm107) Mkoani Rukwa.*



*Barabara ya Mzunguko ya Dodoma (Dodoma outer ring road).*

Ameongeza kuwa miradi yote mikubwa ya ujenzi wa barabara za miji kwa kiwango cha lami lami inahusisha uwekaji wa taa za barabarani akitoa mfano wa barabara yote ya mzunguko wa nje ya jiji la Dodoma ambayo kilometa zote 112 zitawekwa taa za barabarani. Pia katika mwaka huu wa fedha 2025/26, taa za barabarani 5,200 zitawekwa katika kila mkoa katika vijiji na miji takriban 200.

Katika eneo la vivuko, anasema Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imeiwezesha TEMESA kuanza ujenzi wa Vivuko vipya 5 katika Ziwa Victoria na kimoja katika Bahari ya Hindi. Vivuko hivyo vinatarajiwa kukamilika Septemba, 2025 ambavyo ni Kivuko cha Kisorya Rugezi kitakachotoa huduma kati ya Kisorya Wilayani Bunda Mkoani Mara na Rugezi Wilayani Ukerewe Mkoani Mwanza; Kivuko cha Bwiro Bukondo kitakachotoa huduma kati ya Bwiro na Bukondo Wilayani Ukerewe Mkoani Mwanza; Kivuko cha Ijinga na Kahangala Wilayani Magu Mkoani Mwanza; Kivuko cha Nyakarilo Kome mkoani Mwanza na Kivuko cha Buyagu Mbarika mkoani Mwanza, na ujenzi wa Kivuko cha Mafia-Nyamisati unaendelea.

Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), imeendelea kutekeleza baadhi ya miradi ya uendelezaji wa miliki ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za wakaazi 644 wa Magomeni Kota jijini Dar es Salaam; Ujenzi wa nyumba 170 za Watumishi wa Umma katika Mikoa ya Dodoma, Mtwara na Pwani. Ujenzi wa majengo manne (04) ya ghorofa yenye uwezo wa kuchukua familia 66 katika maeneo ya Magomeni Kota (Awamu ya Pili), Masaki jijini Dar es Salaam, na Simeone jijini Arusha na Ujenzi wa nyumba 32 kwa ajili ya Viongozi wa Serikali katika mikoa ya Dodoma, Simiyu, Morogoro, Rukwa na Katavi, na ujenzi wa nyumba Nne (04) za Majaji katika mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Mtwara na Shinyanga.





# Sekta ya Madini, Injini ya Uchumi Inayochanua

Na **Grace Semfuko, MAELEZO**

Tanzania, nchi iliyobarikiwa kwa utajiri wa rasilimali asilia, imeweka sekta ya madini kama kiini cha safari yake ya maendeleo.

Kwa miongo kadhaa, ardhi ya Tanzania imeficha hazina zenye thamani kubwa ambapo sasa, chini ya uongozi mahiri wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hazina hizi zinaanza kuleta mabadiliko makubwa, si tu kwa pato la Taifa, bali pia kwa maisha ya Watanzania wengi.

Safari hii ya mabadiliko imejaa mafanikio na mikakati ya kuvutia inayohakikisha kila tone la jasho la mchimbaji linanufaisha Taifa. Haikuwa rahisi kufika hapa, lakini mabadiliko ya sera na utendaji yamefanya sekta ya madini kuwa injini ya kweli ya uchumi.

Miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita imeshuhudia ongezeko la mchango wa sekta hii katika lato la Taifa, ukipanda kutoka asilimia 7.3 mwaka 2021 hadi asilimia 10.1 mwaka 2024.

Mafanikio haya yameivusha serikali katika lengo lililowekwa na Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ikifanikisha hilo mwaka mmoja kabla ya muda uliopangwa. Takwimu zinaonesha wazi kwamba sekta hii haihusiki tena na uchimbaji wa malighafi pekee, bali imegeuka kuwa nguzo imara ya uchumi wa nchi.
Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa majukumu mahususi, ikiwemo usimamizi thabiti wa ukusanyaji wa maduhuli, uendelezaji wa madini muhimu na mkakati, uwezeshaji wa wachimbaji wadogo, na juhudi za kuongeza thamani ya madini nchini.

Ongezeko la kasi ya ukuaji wa sekta ya madini, kutoka asilimia 9.4 mwaka 2021 hadi asilimia 11.3 mwaka 2023, ni ushahidi tosha wa mazingira wezeshi ya uwekezaji yaliyowekwa na serikali, hasa baada ya kuboresha sheria, kanuni na kupeleka miundombinu muhimu kama umeme migodini.



Matokeo ya maboresho hayo yalionekana moja kwa moja katika mapato ya serikali. Maduhuli kutoka sekta ya madini yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 623.24 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 753.18 mwaka 2023/2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 20.8 ndani ya miaka mitatu.

Katika mwaka wa fedha wa 2024/2025, serikali iliweka lengo la kukusanya Shilingi trilioni moja, na kufikia Mei 14, 2025, Wizara ya Madini ilikuwa imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 902.78, sawa na asilimia 90.28 ya lengo hilo, hatua inayothibitisha utendaji bora na uaminifu katika ukusanyaji wa mapato.

Sekta hii pia inachangia kiasi kikubwa katika uchumi wa fedha za kigeni. Mchango wa madini katika mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi umeimarika kutoka dola za Marekani bilioni 3.1 mwaka 2021 hadi dola za Marekani bilioni 3.55 mwaka 2023. Zaidi ya hayo, kwa upande wa mauzo ya bidhaa zisizo za asilia (non-traditional goods), mchango wa sekta ya madini ulipanda kutoka asilimia 53.8 mwaka 2021 hadi asilimia 56.2 mwaka 2023, ikionesha kuwa madini ni chanzo kikuu cha mapato ya kigeni kwa taifa.



# Uwezeshaji wa Watanzania na Wazawa

Mafanikio ya sekta ya madini yanaonekana pia katika ajira na biashara. Waziri wa Madini, Mhe. Antony Mavunde, anaeleza kuwa sekta hii imeajiri Watanzania wengi, ikiwemo ajira za moja kwa moja na ajira kupitia wakandarasi na watoa huduma. Kati ya ajira 19,356 zilizotengenezwa na kampuni za madini kati ya mwaka 2021 na 2023, asilimia 97.40 ya ajira hizo zilitolewa kwa Watanzania. Hii ni dhihirisho la serikali kutoa kipaumbele kwa wazawa.

Vilevile, kampuni za kitanzania zimepata fursa kubwa za kibiashara migodini. Katika kipindi hicho, zilifanikiwa kuuza bidhaa na huduma zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.5 kati ya dola bilioni 3.9 zote zilizouzwa, sawa na asilimia 92 ya biashara yote migodini. Hii inaonesha jinsi sekta ya madini inavyochangia moja kwa moja katika kukuza uchumi wa ndani.

Serikali ya Awamu ya Sita inatambua mchango wa wachimbaji wadogo na inafanya kila juhudi kuwawezesha. Kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Serikali imefanikiwa kununua mitambo 15 ya uchorongaji miamba, na kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo kwa bei nafuu.

Wachimbaji wadogo 16 tayari wamenufaika na huduma hiyo, ambapo jumla ya mita za mraba 3,450.37 zimechorongwa katika maeneo mbalimbali. Pia, zaidi ya wachimbaji wadogo 471 wamepata mafunzo ya kitaalamu kupitia vituo vya mfano.

# Wachimbaji Wadogo na Masoko ya Madini

Masoko ya madini yameendelea kukua. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2019, idadi ya masoko na vituo vya ununuzi imeongezeka kutoka 42 na 100 mwaka 2020/2021 hadi 43 na 109 mwaka 2024/2025. Hii imeongeza uwazi na urahisi wa biashara.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiangalia mfano wa uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu wakati wa Maonesho ya Saba ya Teknolojia na Uwekezaji kwenye sekta ya madini yaliofanyika Mkoani Geita Oktoba 13, 2024.*



Pia, serikali imerudisha minada ya madini ya vito, baada ya kusitishwa kwa miaka mingi. Minada miwili iliyofanyika Mererani imeuza madini yenye thamani ya shilingi bilioni 2.5, na kuiwezesha serikali kukusanya shilingi milioni 163 kama mrabaha na ada mbalimbali.

Minada ya kitaifa na maonesho ya kimataifa yanatarajiwa kufanyika katika mikoa mbalimbali na Zanzibar, ikifungua fursa mpya kwa wafanyabiashara.

## Utafiti wa Madini kwa Kutumia Teknolojia ya Kisasa

Ili kuhakikisha ukuaji endelevu, Wizara ya Madini inaendelea na maandalizi ya kufanya utafiti wa kina kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kurusha ndege, High Resolution Geophysical Survey. Lengo ni kuongeza eneo lenye taarifa za kijiolojia kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia asilimia 34 ifikapo mwaka 2026.



## Ununuzi wa Dhahabu Kupitia Benki Kuu

Ili kuhakikisha ukuaji endelevu, Wizara ya Madini inaendelea na maandalizi ya kufanya utafiti wa kina kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kurusha ndege, High Resolution Geophysical Survey. Lengo ni kuongeza eneo lenye taarifa za kijiolojia kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia asilimia 34 ifikapo mwaka 2026.









# Awamu ya Sita Yaweka Mazingira Mazuri ya Uendelezaji Viwanda, Biashara



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan akibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi, Mbigiri mkoani Morogoro, Agosti 7, 2024.*

Na **Jonas Kamaleki, Dodoma**

Tanzania sasa imejiandaa vilivyo kujenga uchumi imara na wenye ushindani kupitia sekta ya viwanda na biashara. Chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mazingira mazuri yanayowezesha wawekezaji na wafanyabiashara kustawi.

Lengo kuu la kuikumbatia sekta hii ni kuifanya kuwa injini ya ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira, na kujenga msingi imara wa maendeleo endelevu.

Wakati akihutubia Bunge mwezi Aprili 2021, Rais Samia alisisitiza wazi kuwa maendeleo ya taifa yanategemea sana viwanda. Alitoa wito wa kuvutia uwekezaji ili kuongeza uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya kimataifa, na kupunguza utegemezi wa bidhaa za nje.

Chini ya uongozi wa Rais Samia, ahadi hii inaonekana wazi kutimia kupitia juhudi zinazofanywa na serikali ya sasa ya kuvutia uwekezaji katika viwanda ili kuongeza uzalishaji, ushindani, uwezo wa kuuza bidhaa nje na kupunguza utegemezi wa bidhaa za nje.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Seleman Jafo, amethibitisha kwamba wizara yake ina jukumu la msingi la kuboresha sera na mikakati. Hii inahusisha kuimarisha mifumo ya uratibu na usimamizi. Lengo ni kurahisisha shughuli za kibiashara na uendeshaji wa viwanda, ambavyo vitatumia malighafi za ndani kama mafuta, gesi, saruji, chuma, ngozi, na mazao ya kilimo.

Huu ni mwanzo wa safari ya mabadiliko makubwa ambayo yanalenga kujenga Tanzania yenye uchumi wa viwanda, na hivyo kutoa ajira na kuleta ustawi kwa wananchi wake.



*Kiwanda cha kuchakata pamba cha Biosustain Tanzania Limited kilichopo Meatu mkoani Simiyu ambacho kimezinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Juni 17, 2025.*

Hakika, kutokana na utekelezaji wa majukumu hayo katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara na Taasisi zake 13, ambazo ni BRELA, CAMARTEC, CBE, FCC, FCT, NDC, TIRDO, TEMDO, TANTRADE, WMA, TBS, WRRB, na SIDO, zimeendelea na jitihada mbalimbali za kuendeleza sekta ya viwanda na biashara.

Unyanyuaji wa kisekta unaweza kufikiwa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya 2025, Agenda ya Dunia ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Agenda ya Maendeleo ya Bara la Afrika Tuitakayo 2063.

Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) katika Sekta ya Viwanda na Biashara zinalenga kukuza mazingira rafiki ya biashara, kuvutia wawekezaji (ndani na nje), kuimarisha viwanda, kuchochea ujasiriamali na biashara ya kimataifa, kuboresha miundombinu (nishati na usafiri), kuanzisha maeneo maalum ya kiuchumi, kusambaza uchumi na kuunga mkono kilimo na usindikaji, kukuza minyororo ya thamani.

Waziri Jafo anasema wizara yake itahakikisha kuna kuwepo na maendeleo endelevu, kukuza ukuaji wa kiuchumi na ushindani, kuhamasisha uvumbuzi na teknolojia, kukuza biashara na viwanda vinavyolenga masoko ya nje, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuchochea ujasiriamali (hasa kwa SMEs), na kuhakikisha maendeleo endelevu kwa wananchi na taifa.

Kwa kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara ya Viwanda na Biashara imepata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo uendelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati; Upanuzi na ujenzi wa viwanda. Atamizi na ubunifu; Uendelezaji wa teknolojia mbalimbali; Utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania ndani na nje ya Nchi; Ubora wa bidhaa na ushindani wa kibiashara; na Utatuzi wa migogoro.

Sekta ya viwanda na biashara ni nguzo muhimu ya uchumi, inayochochea maendeleo endelevu kwa kuongeza thamani ya mali ghafi, kutoa ajira, kuongeza mapato, na kuboresha teknolojia. Mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2024 ulikuwa asilimia 7.3 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2023. Aidha, ukuaji wa sekta ya viwanda ulikuwa asilimia 4.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2023.

Vilevile, mchango wa sekta ya biashara katika Pato la Taifa kwa mwaka 2024 ulikuwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2023. Halikadhalika, kasi ya ukuaji wa sekta ya biashara ilikuwa asilimia 4.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2023. Ukuaji huo umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara.

Mafanikio mengine makubwa ni pamoja na ulipaji wa fidia ya Sh bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 kwa ajili ya Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga. Pia, serikali imefanikiwa kumpata mwekezaji mpya, Kampuni ya Shudao Investment Group Company Limited (SDIG), inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Kwa mujibu wa Dkt. Jafo, Wizara kupitia NDC imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kimkakati na kielelezo wa magadi soda uliopo katika bonde la Engaruka wilayani Monduli. Katika mwaka 2024/2025, serikali imetoa jumla ya Shilingi 6,304,672,959 kwa ajili ya mradi huo.

Kati ya fedha hizo, shilingi 5,895,890,224 ni kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi 595 waliopisha mradi na kiasi cha Shilingi 408,782,735 ni kwa ajili ya malipo ya ada ya mwaka ya leseni ya uchimbaji madini.

Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Shilingi 5,702,104,241.70 sawa na asilimia 97 ya fedha zote za zililipwa kwa wafidiwa 528 kati ya wafidiwa 595. Aidha, ukamilishaji wa zoezi la ulipaji fidia wa kiasi kilichobaki cha Shilingi 194,303,812.31 unaendelea kwa wafidiwa 67 waliobaki ambao wanakamilisha nyaraka muhimu zikiwemo taratibu za mirathi.

Wizara kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ilifanikiwa kufufua Kiwanda cha Kilimanjaro Mashine Tools (KMTC) baada ya kusimama kwa zaidi ya miaka 30. Katika kipindi cha miaka minne (4), serikali ilitoa takriban Shilingi bilioni 4.07 kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji, na kufikia sasa mashine 47 na vipuri 132 vimezalishwa.



Kiwanda  cha Sukari Mkulazi kilichopo Mbigiri mkoani Morogoro.





Kiwanda hiki sasa kinategemewa kwa vipuri na viwanda vya ndani kama TPC, Kam puni ya Bia Tanzania (TBL), Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi cha Kilimanjaro (KLICL), viwanda vya mkonge, na mashamba ya maua.

Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea na jitihada za kukiendeleza Kiwanda cha Tanzania Biotech Company Limited (TBPL) kilichopo Mkoa wa Pwani ambacho kinazalisha dawa za kibaiolojia (Bio-Products) za viuadudu vya kuua mazalia ya mbu na viuatilifu hai kwa ajili ya kuua wadudu dhurifu kwenye mazao. Kwa kutumia Shilingi bilioni 5 kununua viuadudu hivyo. Katika miaka minne, kiwanda kimezalisha na kuuza lita 703,608 za viuadudu, ambapo lita 415,164 zimesambazwa katika halmashauri 123 na lita 288,444 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.6 zimeuzwa kwa nchi za Kenya, Angola, Niger, Botswana, Namibia, Eswatini, Mozambique, na Uganda.

Wizara imevutia uwekezaji katika kongani ya viwanda ya Sino Tan Industrial Park, Pwani, inayotarajiwa kuwa na viwanda 500 (200 vikubwa, 300 vidogo) na kutoa ajira 600,000 (100,000 za moja kwa moja, 500,000 zisizo za moja kwa moja) ifikapo 2027. Hadi kufikia Machi 2025 miundombinu mbalimbali imekamilika, viwanda vinne ambavyo ni kiwanda cha nguo cha House of Garments, Kiwanda cha vipodozi cha KVS Chemicals, Kiwanda cha Snowsea kinachozalisha vifaa vya umeme vya majokofu na kabati maalum ya kuhifadhia bidhaa baridi vimeanza uzalishaji, huku wawekezaji sita wengine wakiwa wamesaini mikataba.

Serikali imefanikiwa kuwezesha uanzishaji wa kongani ya kisasa ya viwanda kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 1,077, ambapo eneo hilo limegawanywa katika viwanja 210 ikiwemo viwanja 202 kwa ajili ya viwanda, viwili (2) ni kwa ajili ya vituo vya umeme (54MW) na (400MW), viwili (2) ni vya biashara, vitatu (3) vya huduma za jamii kimoja (1) cha bandari kavu.

Hadi Machi 2025, Viwanda vitano (Sulphur and minerals, Tan smart lyf, Nadeem, Mohamed Maaz Abdul, na TanTurk) vilikuwa katika hatua ya ujenzi, na wawekezaji 11 wamesaini mikataba. Kongani hii itatoa ajira 30,000 za moja kwa moja na 200,000 zisizo za moja kwa moja.

Kongani ya TAMCO ina wawekezaji 14 ambao wameanza uwekezaji na wamesaini mikataba na 7 wanakamilisha maandiko .

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, Tanzania imeshuhudia ongezeko kubwa la viwanda, na kuchangia ukuaji wa uchumi, ajira, na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Bidhaa hizi ni pamoja na vifaa vya ujenzi, plastiki, magodoro, nguo, chakula, vinywaji, chokaa, vioo, vifungashio, betri za magari, vitakasa mikono, luku, transfoma, magari, na



*Kiwanda cha Kuunganisha Malori na Matipa cha Saturn Corporation Limited kilichopo Kigamboni Jijini Dar es Salaam*

pikipiki.

Tanzania ina jumla ya viwanda 13 vya magari, kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili vinaunganisha magari ambavyo ni GF Trucks and Equipment Ltd kilichopo Pwani na Saturn Corporation Limited kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam. Viwanda 11 vilivyosalia vinatengeneza matrela. Kiwanda cha GF Truck kina uwezo wa kuunganisha magari 200 kwa mwezi na kimetoa ajira 300.

Kiwanda cha Saturn Corporation kina uwezo wa kuunganisha vichwa vya magari 900 na tipa 270 kwa mwezi na kimetoa ajira za kudumu 250. Kiwanda cha TATA kitakapokamilika kinatarajia kuunganisha vichwa vya magari, tipa pamoja na pikipiki
.

Kwa upande wa Sekta ya Maendeleo ya Biashara, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 toleo la 2023 pamoja na mkakati wake ambayo ilizinduliwa tarehe 30 Julai, 2024 Dar es Salaam ikiwa na lengo la kutoa mwongozo wa uratibu na ukuaji wa sekta ya biashara nchini kwa kuimarisha maendeleo ya biashara ya ndani; kuimarisha ushirikiano wa biashara za Kikanda na Kimataifa; kuongeza matumizi ya fursa za soko la nje.


CAPITAL
NX 380
SINOTRUK



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Rukwa mara baada ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa shule hiyo iliyopo Laela mkoani humo Julai 17, 2024.*

# Samia Ajenga Shule 26 za Sayansi kwa Wasichana

Na **Paschal Dotto- MAELEZO**

Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya uamuzi muhimu kwa kujenga na kukamilisha shule 26 za sayansi, maalumu kwa ajili ya wasichana katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Hatua hii inaweka msingi imara kwa maelfu ya watoto wa kike ambao wana ndoto za kufikia ngazi za juu kielimu, hususan katika fani za sayansi.

Ujenzi huu mkubwa unalenga kuhakikisha watoto wa kike kote nchini wanapata elimu bora na mahususi itakayowaandaa kuwa wataalamu wa baadaye katika fani za sayansi na teknolojia.

Mafanikio haya ya kihistoria yanahusiana moja kwa moja na utekelezaji wa Sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, iliyozinduliwa rasmi na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Februari 1, 2025. Sera hii inalenga kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu, na ujenzi wa shule hizi 26 unaashiria utekelezaji wa mageuzi hayo, hasa katika uboreshaji wa elimu ya mtoto wa kike.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda anaeleza jinsi mabadiliko ya Sera ya Elimu yanavyokwenda kuleta mageuzi makubwa nchini.

"Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 imeleta mageuzi kwa kuweka elimu ya lazima kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha nne kwa mfumo ufuatao; msingi





miaka 6, kidato cha kwanza hadi cha nne miaka 4, ambapo mwanafunzi anatakiwa kuanza darasa la kwanza akiwa na umri wa miaka 6 baada ya kumaliza elimu ya awali" anasema Prof. Mkenda.

Katika mahojiano kwa nyakati tofauti na wanafunzi wa shule mpya za sayansi kwa wasichana, wamesema mradi huo umekuja wakati muafaka na wanatarajia mageuzi makubwa katika ndoto zao .

"Tunavutiwa kuwepo hapa, mazingira ya masomo yetu ni mazuri na salama kwa mtoto wa kike kupata elimu, tunapata fahari kubwa ya kujifunza na kusoma masomo ya sayansi kwani awali kazi za masomo haya zilionekana ni za wanaume. Lakini kutokana na Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kujenga shule hizi nzuri watoto wa kike wanapata kipaumbele katika fani za sayansi. Wapo tunaotaka kuwa wahandisi, wapo wanataka kuwa madaktari na wengine kuwa wafamasia", anaeleza Rehema Maningu mwanafunzi wa Shule ya Wasichana ya Sayansi Geita.

Neema Baraka wa Shule ya Wasichana ya Sayansi Mara anaeleza jinsi walivyokuwa wanapata ugumu wa kusoma masomo ya sayansi kabla ya serikali kutekeleza mradi wa ujenzi wa shule hizo za wasichana zenye mazingira wezeshi kwa usomaji wa masomo hayo.

"Tupelekee shukrani zetu kwa Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan kwanza kwa kutoa elimu bure pili kwa kujenga shule hizi nzuri maalumu kwa ajili ya sisi watoto wa kike wa nchi hii. Ni shule ambazo kufaulu kwake katika masomo ni kwa uhakika," anasema Janeth Sasi wa Shule ya Wasichana ya Sayansi Mwanza.

Naye Dorice Dioniz wa Shule ya Wasichana ya Sayansi Simiyu akiwa kidato cha kwanza katika shule hiyo maalum anasema:"Shule hii ni mchepuo wa sayansi na ina mazingira mazuri ya kujifunzia itatusaidia katika kutimiza ndoto zetu Ahsante Mama Samia Suluhu Hassan".

Shule hizi 26 zimekuwa mkombozi kwa mtoto wa kike Tanzania, Victoria Henry Dema anamshukuru Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa ujenzi wa



*Shule ya Sekondari ya Wasichana Simiyu*

shule hizo akisema: “Mama Samia ameona watoto wa kike wanaweza masomo ya sayansi na uamuzi wake wa kujenga shule hii ya Kagera River Girls ametuhamasisha sisi wasichana kupambana na kusoma masomo ya Sayansi mimi nasoma tahasusi ya PCB.”

Serikali imetumia kiasi cha Shilingi bilioni 115.7 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari 26 za sayansi kwa wasichana kwa mikoa yote 26 ya Tanzania Bara

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Aldof Mkenda anaeleza kuwa pamoja na mageuzi hayo ya shule 26 za wasichana katika elimu ya mtoto wa kike lakini pia katika kipindi cha miaka minne serikali imeanza ujenzi wa majengo ya madarasa, maabara, mabweni katika kampasi kuu na za pembezoni mpya 16 za vyuo vikuu katika mikoa ambayo haikuwa na taasisi za elimu ya juu.

Mikoa hiyo ni pamoja na Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Tanga, Mwanza, Njombe, Katavi, Rukwa, Tabora, Simiyu, Manyara, Shinyanga, Ruvuma na Singida na Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar ili kuongeza fursa za elimu ya juu kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) wenye thamani ya Shilingi bilioni 972.

Aidha amesema chini ya Serikali ya Awamu ya Sita, mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka shilingi bil. 464 mwaka 2021/22 hadi Shilingi bil. 787 mwaka 2024/25.Serikali pia imeondoa asilimia 16 ya faini na tozo ya urejeshaji wa mikopo hiyo ili watu warudishe kwa wakati na kasi zaidi.

Ndani ya uongozi wa Rais Samia kumeanzishwa programu ya Samia Scholarship inayotoa ufadhili na yenye nia ya kuongeza idadi ya wanafunzi katika masomo ya sayansi waliofaulu vizuri kidato cha sita na kujiunga katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Elimu Tiba na Hisabati .

Kwa hiyo kuwapo kwa muunganiko wa shule 26 za sayansi na ufadhili wa masomo wa Samia Scholarship kutainua sekta ya elimu na kuwezesha uwepo wa wataalamu wa sayansi wa kutosha wanawake kwa wanaume.







Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga




Shule ya Sekondari ya Wasichana Kagera




Shule ya Sekondari ya Wasichana Mara



# Shilingi Trilioni 5.6 Zatumika Kuifungua Mwanza Kiuchumi

Na **Mwandishi Wetu - MAELEZO**

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Jiji la Mwanza ambapo ndani ya kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, jumla ya shilingi trilioni 5.6 zimetolewa kuendeleza sekta za afya, elimu, maji, miundombinu, nishati, kilimo, mifugo, biashara na utawala bora.

## Afya

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda anaeleza kuwa kupitia fedha hizo mkoa wa Mwanza umefanya maboresho makubwa katika sekta ya afya ambapo shilingi bilioni 63.2 zimetolewa kwa ajili ya uboreshaji wa hospitali za wilaya za Ukerewe, Nyamagana na Magu, ujenzi wa wodi ya saratani na ununuzi wa mitambo ya oksijeni katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando, kuimarisha vituo vya kutoa huduma za kibingwa na kununua vifaa vya kisasa kama MRI, CT-Scan, Digital X-Ray na Ultrasound.

Mhe. Mtanda anaeleza kuwa katika kuhakikisha huduma bora kwa wananchi zinaendelea kutolewa, serikali imeongeza idadi ya wataalamu wa afya kutoka 2,855 mwaka 2020 hadi 4,150 mwaka 2025. Pia, upatikanaji wa dawa umeimarika kutoka asilimia 77.89 hadi 92.29. Aidha, katika eneo hilo la afya serikali imefanikiwa kupunguza maambukizi ya malaria kutoka asilimia 8 hadi 1.



## Elimu

Kwa upande wa Sekta ya Elimu, Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 196.8 kugharamia mpango wa Elimu Bila Malipo ambao umetekelezwa kwa mafanikio makubwa katika jiji hilo ambapo shule za msingi zinazonufaika zimeongezeka kutoka 873 hadi 930, huku shule za sekondari zikiongezeka kutoka 219 hadi 308. Kwa upande wa uboreshaji wa mazingira ya elimu, Mhe. Mtanda anaeleza kuwa kupitia fedha hizo serikali imekarabati vyumba vya madarasa na kujenga vipya, kujenga maabara, mabweni na matundu ya vyoo.

## Maji

Mhe. Mtanda anaeleza pia jumla ya shilingi bilioni 264.8 zimetumika katika miradi ya maji, ambapo upatikanaji wa maji mijini umeongezeka kutoka asilimia 57 hadi 85, na vijijini kutoka 57 hadi 77.8.

Vilevile miradi ya maji 80 ya vijijini na 19 ya mijini imetekelezwa, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha Butimba na usambazaji wake.

## Nishati

Kwa upande wa sekta ya nishati,serikali imeupatia Mkoa wa Mwanza shilingi bilioni 110 ili kuimarisha miradi ya upatikanaji wa nishati ya umeme vijijini ambapo jumla ya vijiji 522 na vitongoji zaidi ya 1,800 vimepata huduma ya umeme. Pia, serikali imesambaza nishati mbadala kwa wananchi na taasisi za umma.



*Mradi wa Chanzo na Kituo cha Kutibu Maji cha Butimba uliotekelezwa chini ya Programu ya Maji na usafi wa Mazingira ya Ziwa Victoria.*

## Barabara na Nadaraja

Kwa upande wa miundombinu ya barabara, serikali imetumia Shilingi bilioni 156.3 kuimarisha mtandao wa barabara ndani ya Mkoa wa Mwanza kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) wameboresha mtandao wa barabara, kujenga madaraja likiwemo la Kigongo Busisi, makalavati pamoja na kuweka taa za barabarani ambapo mtandao wa barabara za lami umeongeza kutoka kilometa 76.82 hadi kilometa 103.08

## Usafiri wa Maji na Anga

Aidha, anaeleza kuwa usafiri wa majini na anga umeimarika kwa serikali kujenga vivuko vipya 5 na kukarabati vivuko 12, kujenga meli ya kisasa ya MV Mwanza ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 96 pia kufanyia maboresho Uwanja wa Ndege wa Mwanza na ujenzi wa jengo la abiria.

## Kilimo

Kwa upande wa sekta ya kilimo na mifugo, Mkoa wa Mwanza umepata mafanikio kwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula ambao umefikia tani 385,000, usambazaji wa mbolea na viuatilifu kupitia ruzuku na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji ya Sengerema na Kwimba.

Pia idadi ya mifugo imeongezeka kwa kiwango kikubwa ambapo uzalishaji wa mitamba umepanda kutoka mitamba 58,625 mwaka 2020 hadi 215,775 mwaka 2025 sawa na ongezeko la mitamba 157,149. Aidha, katika kuhakikisha mifugo iliyopo inakingwa na magonjwa mbalimbali, serikali imejenga majosho mapya hatua iliyoongeza idadi ya majosho kutoka 55 ya mwaka 2020 hadi 76 mwaka 2025 ambayo ni sawa na ongezeko la majosho 21.

## Uvuvi

Katika sekta ya uvuvi, idadi ya vizimba vya kisasa vinavyotumika kufugia samaki imeongezeka kutoka 1,664 hadi 2,715. Ongezeko hilo limeongeza mapato ya uvuvi kutoka shilingi bilioni 4.4 mwaka 2020 hadi bilioni 8.2 mwaka 2025.

## Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Katika eneo la uwezeshaji wananchi kiuchumi, serikali imeendelea kutoa mikopo ya asilimia 10 isiyo na riba kwa vikundi imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 3.3 hadi 14.1. Vilevile, kaya 59,932 zimenufaika kupitia TASAF.

## Viwanda

Kwa upande wa sekta ya viwanda idadi ya viwanda vikubwa imeongezeka kutoka 46 mwaka 2020 hadi viwanda 50 mwaka 2025 sawa na ongezeko la viwanda 4, hali kadhalika idadi ya viwanda vya kati imeongezeka kutoka 109 mwaka 2020 hadi viwanda 116 mwaka 2025. Idadi ya viwanda vidogo na vidogo sana imeongezeka kutoka viwanda 1,776 mwaka 2020 hadi viwanda 2,322 kwa Mwaka 2025 sawa na ongezeko la viwanda 546.




*Baadhi ya Boti za kisasa zilizokabidhiwa kwa wavuvi mkoani Kigoma.*



# Uimara wa JWTZ Wawezesha Tanzania Kuwa Kisiwa cha Amani

Na **Paschal Dotto - MAELEZO**

Tanzania inaendelea kudhihirisha hadhi yake kama kisiwa cha amani na utulivu katika bara la Afrika. Chini ya uongozi mahiri wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu, Serikali imeweka mkazo mkubwa katika kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka , wananchi, na mali zao. Mafanikio haya yamekuwa nguzo kuu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii
.

Ili jeshi kuendelea kutekeleza wajibu wake serikali imeongeza bajeti kwa vikosi vya ulinzi na usalama, hasa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Uwekezaji huu umewezesha jeshi kupatiwa vifaa na zana za kisasa, na pia kuwezesha mafunzo na mazoezi ya hali ya juu. Mafunzo haya yamejumuisha mazoezi ya kimataifa na majeshi mengine.

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, JWTZ imefanya mafunzo na mazoezi ya utayari ikiwemo zoezi la 'Shared Accord', 'Beach Landing Operation', 'Joint Combined Exchange Training (JCET)', Linda Kisiwa, Linda Mpaka, 'Dragon Fly na Kaa Tayari pamoja na zoezi la utayari na Jeshi la Ukombozi la Watu wa China mwaka 2023.

Mazoezi mengine ni lile la kupambana na uharamia majini lijulikanalo kama 'Amphibious Assault', zoezi la Amani Umoja 2024, zoezi lijulikanalo kama

‘Africa India Key Maritime Engagement 2025’ na zoezi la kuimarisha na kuwajengea uwezo maafisa na askari liitwalo ‘Cutlass Express’ lililohusisha majeshi ya mataifa 14.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dkt. Stergomena Tax, amesisitiza kuwa uimarishaji wa JWTZ umechangia pakubwa katika kudumisha amani na utulivu, hali iliyochochea maendeleo ya kiuchumi.

JWTZ halijafanikiwa katika medani za kijeshi pekee, bali pia katika miradi ya ujenzi wa kitaifa. Jeshi letu limekuwa mstari wa mbele katika ulinzi na ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwemo ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, mradi wa JNHPP, ulinzi wa Reli ya SGR, na hata mradi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanga.

Aidha, anaeleza kuwa ili kuwezesha ufanisi zaidi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa – MMUT katika eneo la Kikombo, Jijini Dodoma unaogharamiwa na Serikali na kutekelezwa na wataalam wa ndani ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 93.5. Pia JWTZ inaendelea na ujenzi wa Hospitali kuu ya Kanda Dodoma yenye hadhi ya daraja la nne inayojengwa katika eneo la Msalato katika Jiji la Dodoma kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani, Ujenzi wa hosteli za Chuo cha Taifa cha Ulinzi na kujenga makazi ya wakufunzi na waalimu waelekezi wa chuo cha ukamanda na unadhimu Arusha.

Pia, wizara inaendelea na ujenzi wa makazi ya askari wa JWTZ, hospitali Kuu ya Jeshi - Mwanza na Chuo cha TMA – Arusha pamoja na ujenzi wa Makao Makuu ya Kamandi ya Jeshi la Akiba mkoani Singida.

Aidha, Wizara ya Ulinzi na JKT imefanya tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia ikiwemo utengenezaji wa bomu la kufukuzia tembo. Teknolojia zingine zilizohaulishwa ni pamoja na ubunifu wa kuzalisha magari ya deraya, utengenezaji wa “chasis” za magari ya Nyumbu na Zimamoto na utengenezaji wa mashine mbalimbali kwa ushirikiano na TAWIRI, COSTECH na TIRDO.

Waziri Tax anaeleza kuwa Serikali imeweza kuimarisha mashirika ya umma ya kijeshi kwa kujenga miundombinu ya milki, kuanzisha Karakana Kuu ya kukalibu chuma, kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mazao ya msingi yatakayotumiwa na vyombo vya ulinzi, ujenzi wa karakana ya kukarabati silaha ndogo na ununuzi wa mashine na mitambo mipya.

Serikali pia imetoa mafunzo ya mujibu wa sheria kwa vijana 143,863, vijana wa kujitolea 46,196, na mafunzo ya mgambo kwa vijana 55,790. Mafunzo haya yanajenga nidhamu na uzalendo, huku yakitayarisha vijana kwa ajira na utumishi wa umma.





Wizara ya Ulinzi pia imefanya utafiti wa kina na kuhamisha teknolojia, ikizindua miradi bunifu kama utengenezaji wa bomu la kufukuzia tembo, magari ya kivita ya deraya, na mashine mbalimbali kwa ushirikiano na taasisi za ndani. Uwezo huu wa kiubunifu unaimarisha uwezo wa kujitegemea wa jeshi letu na kuchangia katika uchumi wa viwanda.

Hadi kufikia Juni, 2025, Shirika la Maendeleo ya Jeshi (SUMAJKT) limeimarisha viwanda vyake, ikiwemo kiwanda cha maji Mgulani kinachozalisha katoni 2500 kwa siku na kiwanda cha nguo kinachoshona mavazi 300 hadi 400 ya kijeshi kwa siku. Uwekezaji huu unaongeza uzalishaji, unapunguza utegemezi wa bidhaa za nje, na kuimarisha uchumi wa nchi.

Kwa ujumla, juhudi hizi zinaonesha wazi kwamba ulinzi na maendeleo ni pande mbili za shilingi moja. Uimara wa jeshi letu ndio unawezesha wananchi wetu kuishi kwa amani, kufanya shughuli zao bila hofu, na kuchangia katika ujenzi wa uchumi wa taifa. Hii ndio Tanzania ya amani, utulivu, na maendeleo.














# Shilingi. Trilioni 1.34 Zachochea Ustawi wa Wananchi Katavi

Na **Frank Mvungi, MAELEZO**

Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa mikoa iliyopata fedha nyingi za maendeleo katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Katika kipindi hicho zaidi ya shilingi trilioni 1.3 zimetolewa na serikali ili kuwezesha ukuaji wa uchumi, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, kuboresha maisha na ustawi wa jamii, kuimarisha utawala bora na uwajibikaji ndani ya mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mhe. Mwanamvua Mrindoko anaeleza kuwa kutokana na fedha hizo mkoa huo umeshuhudia mabadiliko makubwa katika uchumi wake na wa wananchi wake.

## Elimu

Akizungumzia sekta ya elimu anaeleza kuwa mkoa huo umepokea Shilingi bilioni 58 kuboresha miundombinu ya shule mbalimbali na kuweka mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunza. Serikali imewezesha ujenzi wa shule mpya 137 zikiwemo 97 za msingi na 40 za sekondari, madarasa 2,219, na uboreshaji wa vyoo 2,734 kwa shule hizo.

Hii imepunguza kwa kiasi kikubwa umbali wa kutembea kwenda shule na msongamano wa wanafunzi madarasani na kuwezesha mazingira bora zaidi kwa walimu na wanafunzi. Aidha, anaeleza kuwa idadi ya shule za sekondari imeongezeka kutoka 39 mwaka 2021 hadi 79 mwaka 2025 sawa na ongezeko la shule 40. Sanjari na hilo, madarasa yameongezeka kutoka 579 mwaka 2021 hadi 1,138 mwaka 2025 ambayo ni sawa na ongezeko la madarasa 559.

Kwa upande wa nyumba za walimu anasema zimeongezeka kutoka 191 mwaka 2021 hadi 225 mwaka 2025 sawa na ongezeko la nyumba 34 . Mhe. Mrindoko anaeleza kuwa maboresho hayo

yameenda sambamba na ongezeko la idadi ya walimu walioajiriwa katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari ambapo katika shule za msingi wameongezeka kutoka walimu 2,321 mwaka 2020 hadi walimu 2,876 mwaka 2025 na shule za sekondari kutoka walimu 726 mwaka 2020 hadi 1,150 mwaka 2025.

Kwa upande wa sekta ya afya, Mhe. Mrindoko anaeleza kuwa serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 41.6 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya, ununuzi wa vifaa na vifaa tiba, ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa, ujenzi wa hospitali 4 za wilaya, ujenzi wa vituo vya afya 11, zahanati 47, ukarabati wa hospitali kongwe (Mpanda MC) na ukarabati wa vituo vya afya na zahanati
.

Anaeleza kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2025 mkoa huo umefikisha jumla ya vituo 161 vinavyotoa huduma za afya ambapo kati ya hivyo ipo hospitali moja ya rufaa ya mkoa, hospitali tano za halmashauri, vituo vya afya 28 na zahanati 127.

Aidha, Zahanati zimeongezeka kutoka 80 mwaka 2021 hadi 127 mwaka 2025 sawa na ongezeko la zahanati 47 na vituo vya afya vimeongezeka kutoka 17 mwaka 2021 hadi kufikia 28 mwaka 2025 sawa na ongezeko la vituo 11 sawa na asilimia 39.

Kwa upande wa maendeleo ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, serikali imetoa Shilingi bilioni 18.38 kukamilisha miundombinu ya jengo la huduma za wagonjwa wa nje, huduma za mama na mtoto, vipimo vya radiolojia na vyumba vya upasuaji. Kwa upande mwingine, ujenzi wa jengo la 'Dialysis" (Huduma ya kusafisha Damu) umekamilika kwa asilimia 100 na huduma zimeanza kutolewa. Pia serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la huduma za dharura (EMD), jengo la wagonjwa mahututi (ICU), ununuzi wa mashine ya CT-Scan, ununuzi wa mashine mbili za kisasa za mionzi (digital X-Ray) pamoja na ununuzi wa vifaa tiba mbalimbali.

Kwa upande wa watumishi wa kada ya afya, Mhe. Mrindoko anaeleza kuwa mwaka 2021, mkoa huo ulikuwa na jumla ya watumishi 898 ambapo hadi kufikia Juni 2025 idadi hiyo imeongezeka na sasa kuna jumla ya watumishi 1,754. Idadi hii inajumuisha watumishi wapya 262 walioajiriwa na serikali mwezi Septemba – Disemba 2024 pamoja na watumishi 98 waliojiriwa kwa mikataba kwenye miradi mbalimbali ya afya ambayo ni sawa na ongezeko la watumishi 856.



*Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi iliyopo Mpanda*

Kwa upande wa sekta ya maji Mkoa wa Katavi umeendelea kutekeleza miradi ya maji yenye thamani ya Shilingi bilioni 32.16 ambayo ikikamilika itaongeza upatikanaji wa maji kwa zaidi ya asilimia 100. Aidha, Mkoa wa Katavi unaendelea kutekeleza mradi wa usambazaji maji kutoka Bwawa la Milala unaotekelezwa chini ya mpango wa ujenzi wa mradi wa Maji wa Miji 28. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba 2025 na utakuwa na uwezo wa kuzalisha maji lita 12,000,000 kwa siku na kunufaisha wakazi wote wa Manispaa ya Mpanda.

Kuhusu sekta ya nishati Mhe. Mrindoko anaeleza kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2025 Mkoa wa Katavi ulikuwa umeunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa na wananchi wa Wilaya ya Mlele, Halmashauri ya Nsimbo na Wilaya ya Tanganyika wanapata umeme wa uhakika. Serikali imetoa shilingi bilioni 116 kugharamia mradi huu kutoa umeme wa 132KV kutoka Mkoa wa Tabora hadi Katavi. Mradi huo umehusisha ujenzi wa njia kubwa ya umeme ya msongo wa Kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Katavi umbali wa kilomita 383 na kujenga vituo viwiwli vya kupoozea Umeme katika eneo la Inyonga kituo chenye ukubwa wa 12MW na eneo la Mpanda kituo chenye ukubwa wa 28MW.

Mhe. Mrindoko anaongeza kuwa serikali imeupatia mkoa huo jumla ya Shilingi bilioni 196.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme ikiwemo upanuzi wa mtandao wa umeme kwa Wilaya ya Mpanda, Tanganyika na Mlele, kuongeza nguvu ya umeme kwa Wilaya ya Mpanda, Tanganyika na Mlele, kupeleka Umeme kwenye Vijiji kwa ufadhili wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) awamu ya kwanza katika vijiji vyote 172 vya Mkoa wa Katavi.

Hadi kufikia Juni, 2025 jumla ya vitongoji 504 kati ya vitongoji 912 vya Mkoa wa katavi vimeunganishiwa umeme na vitongoji 408 vilivyo baki vitaunganishwa katika bajeti hii ambayo utekelezaji wake unaendelea.

Upelekaji wa huduma hizi umeongeza idadi ya wateja wanao tumia umeme kutoka wateja 23,312 mwaka 2020/21 hadi wateja 42,567 Juni, 2025 na kumeleta chachu ya ongezeko la mapato kutoka Shilingi milioni 494.4 hadi Shilingi bilioni 1.03 kwa mwezi, kuongeza uchakataji wa mazao ya kilimo na idadi ya viwanda kutoka 873 mwaka 2021 hadi 1,782 mwezi Juni, 2025.



*Kituo cha Kupokea na Kupoza umeme wa Gridi ya Taifa cha Inyonga mkoani Katavi.*

Kwa upande wa sekta ya barabara hadi kufikia mwezi Juni, 2025 mkoa huo ulipokea kiasi cha shilingi bilioni 63.94 ili kujenga barabara zenye urefu wa kilometa 17.6 kwa kiwango cha lami, kilometa 475 za kiwango cha changarawe, kufungua barabara mpya zenye urefu wa kilometa 487, ujenzi wa madaraja ya kati 31, ujenzi wa makalavati ya kawaida 672 na ujenzi wa madaraja ya mawe 20 ambayo yote yamekamilika.

Kwa upande wa usafiri wa anga Mhe. Mrindoko anaeleza kuwa Mkoa wa Katavi ulipokea Shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na abiria ambalo tayari limekamilika na linatumika. Pia Mkoa una huduma ya uhakika ya usafiri wa anga kati ya Mpanda na Dar - es- Salaam ambao unafanywa mara tatu kwa siku za Jumatatu, Alhamisi na Jumamosi kwa wiki kupitia Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL). Uwepo wa uhakika wa safari za ndege kupitia shirika hilo, umerahisisha mawasiliano na kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa mkoa huo.

Kwa upande wa sekta ya kilimo, serikali imeendela kuhakikisha upatikanaji wa mbolea ya ruzuku ambapo tani 21,953 za mbolea zilizotolewa zimewanufaisha wakulima wapatao 30,109. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kununua vitendea kazi ikiwemo gari moja, pikipiki 72 na vipima udongo 5 na vishikwambi 91 kwa ajili ya maafisa ugani.

Maboresho haya yameimarisha usalama wa chakula kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 990,629 mwaka 2021 hadi tani 1,286,905 mwaka 2025, Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya biashara ya kimkakati kutoka tani 40,057 mwaka 2021 hadi tani 77,898 mwaka 2025.

Sekta ya Mifugo, imeendelea kuimarika ndani ya kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo hadi kufikia Juni, 2025 sekta ya mifugo imepata zaidi ya shilingi bilioni 1.5 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za mifugo ikiwemo majosho, mabirika, malambo, vibanio na sambamba na kusambaza dawa za kuogesha mifugo zenye ruzuku ya serikali katika majosho yote yanayofanya kazi.



*Maboresho ya  Jengo la abiria na Kiwanja cha Ndege cha Mpanda mkoani Katavi.*




*Vihenge na Maghala ya Kisasa kuhifadhia Nafaka ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi wa Chakula (NFRA) Mpanda mkoani Katavi.*

Huduma za umwagiliaji zimeendelea kuimarika ndani ya Mkoa wa Katavi kupitia  ukarabati wa Skimu za Mwamkulu na Kabage kwa gharama ya Shilingi bilioni 54.68 ambazo utekelezaji wake umefikia asilimia 22.5. Kukamilika kwa skimu hizo kutaongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 2,700 hadi hekta 6,000 na kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka gunia 10 hadi wastani wa gunia 60, eneo la umwagiliaji limeongezeka kutoka hekari 36,687 mwaka 2021 hadi hekari 267,680 mwaka 2025.

Kazi nyingine iliyofanyika ni kuimarisha ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kutoa mafunzo kwa vijana 756 kuhusu ujenzi wa vitalu nyumba, kuongezeka kwa vyama vya ushirika kutoka 36 vyenye wanachama 18,340 mwaka 2021 hadi vyama vya ushirika 56 vyenye wanachama 25,320 mwaka 2025.

Kwa hiyo katika miaka minne tu ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, mkoa wa Katavi umegeuzwa na kuwa kitovu cha maendeleo. Fedha zilizotolewa za zaidi ya Shilingi trilioni 1.34 zimekuwa siyo takwimu tu, bali zimeleta mabadiliko ya kweli kwa wananchi. Tunaona shule zikijengwa, vituo vya afya vikifunguliwa, barabara zikipitika, na umeme ukiwaka katika maeneo ambayo awali yalikuwa gizani. Mafanikio haya yamefungua fursa za kiuchumi, yameimarisha ustawi wa jamii, na yametoa matumaini mapya kwa wakazi wa Katavi. Ni dhahiri kuwa Katavi ya sasa siyo Katavi ya jana; ni mkoa unaosonga mbele kwa kasi, ukiwa umeshikilia dhamira ya kujenga Tanzania yenye maendeleo shirikishi na endelevu kwa wote.



*Skimu ya Umwagiliaji ya Mwamkulu iliyopo kijiji cha Mwamkulu mkoani Katavi.*

# Trilioni 11.4 Zawasha Moto wa Maendeleo Kigoma



Soko la pamoja la Mpakani mwa Tanzania na Burundi (Mnanila).

Na **Mwandishi Wetu - MAELEZO**

Mkoa wa Kigoma, uliopo magharibi mwa Tanzania, sasa una sura mpya ya maendeleo. Katika miaka minne ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, mkoa huu umepokea uwekezaji mkubwa wa Shilingi trilioni 11.4.

Fedha hizo zimewasha moto wa maendeleo, zikifungua fursa na kubadilisha maisha ya wananchi moja kwa moja. Mabadiliko haya ni ushahidi kwamba ahadi za serikali zimefika na zinagusa jamii nzima.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Balozi mstaafu Simon Sirro, akifafanua jinsi fedha hizi zilivyotumika alisema, kiasi kikubwa cha shilingi trilioni 9.4 kimetumika katika ujenzi wa Reli ya SGR kuanzia Tabora hadi Kigoma na Uvinza hadi Msongati-Burundi.

Mradi huu unaiunganisha Kigoma na dunia, ukiitoa kwenye hali ya kutengwa na kuifanya kuwa kitovu cha biashara na uchumi.

> "Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, Mkoa wa Kigoma ulipokea jumla ya shilingi trilioni 11.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusisha ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Tabora hadi Kigoma na Uvinza hadi Msongati-Burundi ambapo kiasi cha Shilingi trilioni 9.4 zilitumika,"
>
> **Mhe. Balozi Mstaafu Simon Sirro, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma**



Kikundi cha Wanawake cha Ntihalizwa kilichopo Halmashauri ya Mji wa Kasulu mkoani Kigoma.

Kando na reli, shilingi bilioni 731.5 zimetumika kuboresha mtandao wa barabara, huku Shilingi bilioni 589.9 zikienda kwenye ukarabati na ujenzi wa meli na Shilingi bilioni 501.7 zimetumika kuimarisha sekta ya nishati.

Miradi mingine mikubwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya afya, shule, na uwanja wa ndege wa Kigoma, ambao umetengewa shilingi bilioni 40. Balozi Sirro alisisitiza kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unaendelea na tayari matunda yake yanaonekana.

Kwa upande wa miundombinu ya barabara, Mhe. Balozi Sirro amesema katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita barabara kuu za vijijini na mijini zimeboreshwa, madaraja na makalavati yamejengwa huku taa za barabarani zikiwekwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Aidha, amesema ujenzi wa barabara ya Kasulu–Kabingo umefikia asilimia 93 ya utekelezaji, huku barabara nyingine kadhaa ndani ya wilaya za mkoa zikiendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

## Uwezeshaji wa wananchi Kiuchumi

Licha ya uwekezaji mkubwa katika miundombinu, Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mkazo katika kumwinua mwananchi wa kawaida. Balozi Sirro akitaja mafanikio makubwa katika uwezeshaji wa kiuchumi, alisema shilingi bilioni 6.4 zimetolewa kama mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu. Mikopo hiyo imekuwa chachu ya kukuza biashara ndogondogo na kuwapa wananchi mtaji wa kujikwamua kiuchumi.

Vilevile, idadi ya kaya masikini katika mpango wa TASAF imepungua kwa kiasi kikubwa, kutoka kaya 112,887 mwaka 2020 hadi 42,194 mwaka 2025. Ongezeko la fedha za TASAF kutoka shilingi bilioni 45.3 hadi 61.5 limechangia pakubwa katika kunusuru maisha ya watu wengi.

## Afya

Katika sekta ya afya, Mkoa wa Kigoma umeongeza huduma kwa kuanzisha hospitali mpya tano za wilaya, kujenga zahanati mpya na kuimarisha upatikanaji wa dawa kutoka asilimia 86 hadi 92. Aidha, Mkoa huo unatekeleza mradi

mkubwa wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Kigoma, sambamba na maandalizi ya Hospitali ya Kanda.

## Elimu

"Kwa upande wa elimu, shule za msingi zimeongezeka kutoka 664 hadi 742 na shule za sekondari kutoka 194 hadi 256. Vyuo vya VETA vimeongezeka kutoka kimoja hadi vinne, na uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 17 na 34. Vilevile, vifaa vya elimu, maabara, madarasa na nyumba za walimu vimeboreshwa kwa kiwango kikubwa." anafafanua Balozi Sirro.

## Maji

Balozi Sirro ameeleza kuwa, huduma ya maji safi mkoani Kigoma imeimarika kutoka asilimia 67.9 hadi 77, huku visima 101 vikiwa vimechimbwa. Miradi 91 ya maji imekamilika na imewanufaisha watu zaidi ya milioni 1.4.

## Umeme

Kwa upande wa upatikanaji wa nishati ya umeme, Balozi Sirro ameeleza kuwa Mkoa wa Kigoma kwa sasa umeunganishwa na Gridi ya Taifa kupitia njia ya msongo wa kati wa kilovolti 33 na kuwezesha vijiji vyote 306 kuunganishwa na umeme, hali iliyoleta mapinduzi katika shughuli za kiuchumi na Kijamii.



# Viwanda na Uwekezaji

Mabadiliko ya miundombinu yameleta mapinduzi katika sekta nyingine. Mkoa ambao kwa sasa umeunganishwa na gridi ya Taifa, na vijiji vyote 306 kuwa na umeme, mazingira hayo yanachochea sekta ya viwanda

Kigoma kwa sasa kuna viwanda vikubwa vinne vimeanzishwa, na maeneo zaidi ya hekta 19.5 yametengwa kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, eneo maalumu la uwekezaji (Kigoma Special Economic Zone KiSEZ) limevutia wawekezaji tisa katika viwanda vya saruji, nondo, asali, nguo na nishati.

# Utalii

Katika sekta utalii, kumekuwa na ongezeko la wageni wanaotembelea vivutio mbalimbali vya mkoa huo ambapo idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kutoka 630 mwaka 2020 hadi 11,769 mwaka 2025. Vilevile, Hifadhi za Gombe, Mahale na Dkt. Livingstone Ujiji vimeendelea kuvutia wageni wa ndani na nje.

# Kilimo

Ametaja mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula kwa asilimia 17 na mazao ya biashara kwa asilimia 9. Aidha, kiasi cha matumizi ya mbolea kimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 85, huku uzalishaji wa mbegu bora za chikichi ukiimarika.

Balozi Sirro amemshukuru Rais Samia kwa jicho la kipekee aliloutupia Mkoa wa Kigoma na akawakaribisha wawekezaji kwenda kuwekeza. Maendeleo haya yote yanaonesha wazi kwamba Kigoma ya leo ni mkoa uliofunguka na ulio tayari kuwa kitovu cha biashara na maendeleo kwa ukanda mzima wa Magharibi mwa Afrika Mashariki.



*Shamba la Chikichi*



# Shinyanga Yang'ara Miaka Minne ya Rais Samia

Na **Mwandishi Wetu - Dodoma**

Mkoa wa Shinyanga uliopo Kaskazini – Magharibi mwa Tanzania na Kusini mwa Ziwa Victoria umeendela kustawi kwa kasi na kuinuka kiuchumi kufuatia uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Mboni Mhita anaeleza kuwa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia, Mkoa huo umeshuhudia mageuzi makubwa ya kiuchumi kufuatia serikali kutoa Shilingi trilioni 1.56 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ambapo kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 79.1 zilielekezwa katika sekta ya afya kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya.

Amesema uwekezaji huo umechochea mafanikio zaidi katika sekta ya afya ikiwemo ongezeko la hospitali za wilaya kutoka 2 mwaka 2020 hadi 7 mwaka 2025 katika maeneo ya Shinyanga DC, Msalala DC, Ushetu DC, Shinyanga MC na Kishapu DC, vituo vya afya kutoka 25 mwaka 2020 hadi 38 mwaka 2025 na zahanati kutoka 226 mwaka 2020 hadi 277 mwaka 2025. Aidha, amesema mkoa huo umenufaika na ongezeko la watumishi wa kada ya afya kutoka 2,104 mwaka 2020 hadi 2,812 mwaka 2025 ikiwa ni sawa na watumishi wapya 708.

Kwa upande wa sekta ya elimu Mhe. Mboni Mhita amesema serikali imetoa Shilingi bilioni 155.24 ili kujenga miundombinu ya elimu na kuongeza idadi ya walimu , ongezeko la shule za msingi kutoka 682 mwaka 2020 hadi 711 mwaka 2025 na shule za sekondari kutoka 186 hadi 200.

Mhe. Mhita ameeleza kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020/2025 mkoa huo umeshuhudia ongezeko la mabweni mapya kutoka 78 hadi 131, maktaba kutoka 9 hadi 31 na ongezeko la walimu wapya 1,215 na kufanya idadi ya walimu sasa kufikia 7, 627.

Kwa upande wa huduma za maji Mhe. Mhita amesema mkoa huo umepokea Shilingi bilioni 113.33 kwa ajili ya usambazaji wa huduma za maji hatua iliyoimarisha upatikanaji wa maji safi na salama mijini kutoka asilimia 63 mwaka 2020 hadi 79 mwaka 2025 na vijijini kutoka asilimia 51 mwaka 2020 hadi 68 mwaka 2025. Aidha, amesema miradi 64 ya usambazaji wa maji imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi huku serikali ikiendelea kutekeleza mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria katika vijiji 111 katika wilaya za Kishapu, Shinyanga na Kahama.

Kwa upande wa sekta ya kilimo, Mhe. Mhita amesema serikali imeendelea kuipa uzito kwa kuwahimiza wakulima kuachana na kilimo duni kisicho na tija na kugeukia kilimo cha kisasa.

"Katika sekta ya kilimo, tumeimarisha upatikanaji maji mashambani kwa kujenga skimu za umwagiliaji kutoka 2 zilizokuwepo mwaka 2020 hadi skimu 15 mwaka 2025 katika halmashauri za Wilaya ya Shinyanga, Shinyanga Mjini, Kahama, Msalala na Kishapu na ujenzi wa bwawa ya umwagiliaji la Nyida na Malenge unaoendelea kwa gharama ya Shilingi bilioni 16.2"

Amesema uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 797,000 mwaka 2020 hadi tani 1,313,073 mwaka 2025 na mazao ya biashara kutoka tani 99,250 mwaka 2020 hadi tani 170,673 mwaka 2025 kufuatia upatikanaji mbolea ya ruzuku ndani ya mkoa huo .Pia kuna ongezeko la matumizi ya mbolea kwa shughuli za kilimo kutoka tani 5,443 mwaka 2020 hadi tani 9,909 mwaka 2025.

Katika hatua nyingine Mhe. Mboni amesema sekta mifugo imepata maendeleo makubwa kwa kuongeza kiwango cha uzalishaji wa maziwa kutoka lita 10,031,225 mwaka 2020 hadi 18,335,300 mwaka 2025 na uzalishaji wa nyama kutoka tani 3,150 hadi 5,600.

Kwa upande wa sekta ya madini amesema uwekezaji uliofanywa na serikali katika sekta ya madini umeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza uzalishaji wa madini kutoka tani 7.9 mwaka 2020 hadi tani 42.5 mwaka 2025.

Aidha amesema mapato ya fedha za kigeni zitokanazo na madini yameongezeka kutoka Dola milioni 44.33 hadi Dola milioni 191.15 na mapato ya Halmashauri yatokanayo na madini yameongezeka kutoka Shilingi milioni 745.4 hadi Shilingi bilioni 3.334.

Hali kadhalika ameeleza kuwa kuna maendeleo makubwa katika sekta ya miundombinu ya barabara, nishati na viwanda


*Bwawa la Nyida mkoani Shinyanga*

kati ya mwaka 2020 – 2025.Mkoa umetumia Shilingi bilioni 221.19 kupanua miundombinu ya barabara, kujenga madaraja na makalavati ili kuimarisha shughuli za maendeleo ya jamii.

"Barabara za lami zimeongezeka kutoka kilometa 224 hadi 281 pia barabara za changarawe zimeongezeka kutoka kilometa 957.11 hadi 1,411.50 na madaraja yameongezeka kutoka 45 hadi 57 kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025" amesema Mhe. Mhita.

Katika eneo la nishati Mhe. Mboni amesema shilingi bilioni 492 zilipokelewa na mkoa kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambapo mafaniko yaliyopatikana ni kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma ya umeme kwa vijiji vyote 506 na vitongoji 982 na kufikisha idadi ya vitongoji 2,704 vyenye huduma ya umeme kwa sasa.

Aidha, miradi 133 ya usambazaji umeme imekamilika na imeanza kutoa huduma na katika nishati safi ya kupikia Mkoa umeendelea kutekeleza mfumo wa nishati safi ya kupikia kwa kutoa elimu na usambazaji wa mitungi 6,500 ya gesi ili kutunza mazingira na kulinda afya za wananchi.

Hali kadhalika maendeleo katika eneo la viwanda na biashara yametajwa kushamiri zaidi chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ambapo Mkoa wa Shinyanga umeanzisha viwanda vikubwa 4 na kuongeza idadi ya viwanda kutoka 36 mwaka 2020 hadi 40 mwaka 2025, viwanda vya kati 12 kutoka 180 hadi 192 mwaka 2025 na viwanda vidogo 222 kutoka 999 mwaka 2020 hadi viwanda 1,225 mwaka 2025. Mhe. Mboni amesema hatua hizo zimechochea ongezeko la ajira za viwandani kwa zaidi ya wananchi 50,000 ambao wameajiriwa na ajira elfu 35,000 kati ya hizo ni za muda na 15,000 elfu ni ajira za kudumu.



*Mradi wa kuzalisha Umeme wa Jua Kishapu mkoani Shinyanga.*

# Simiyu Inavyofunguka kwa Uwekezaji wa Serikali



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu akiwa kwenye picha ya pamoja na Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Simiyu iliyopo Bariadi mkoani Simiyu mara baada ya kufunguliwa Juni 16, 2025.*

Na **Naishoki Makeseni – MAELEZO**

Mkoa wa Simiyu unaojulikana kwa mandhari nzuri, ardhi nzuri yenye rasilimali na utajiri unaovutia kwa shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda umeshuhudia ustawi mkubwa wa kiuchumi katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mkoa huo wenye idadi ya watu 2,140,497 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 umeendelea kuimarika kiuchumi kufuatia uwekezaji mkubwa katika sekta za afya, elimu, maji, kilimo, mifugo, nishati, ujenzi, madini, uchukuzi na viwanda na Biashara.

Mkuu wa Mkoa Simiyu, Mhe. Anamringi Macha anaeleza kuwa hali ya uchumi imezidi kuimarika kufuatia kukua kwa pato la mkoa ambalo limeongezeka kutoka shilingi trilioni 2.5 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 3.5 mwaka 2024. Anaeleza kuwa pato la mtu mmoja mmoja pia limeongezeka kutoka shilingi milioni 1.096 kwa mwaka 2020 hadi shilingi milioni 1.53 mwaka 2024.

## Elimu

Katika sekta ya elimu kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025 jumla ya shilingi bilioni 119.91 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu mbalimbali ya elimu katika shule za msingi na sekondari

.

Aidha, amesema mafanikio mengi yamepatikana katika sekta ya elimu ikiwemo ongezeko la bajeti ya elimu bila ada katika elimu ya msingi na sekondari kutoka Shilingi bilioni 6.81 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 37.75 mwaka 2025, ongezeko la shule za msingi kutoka 513 mwaka 2020 hadi 611 mwaka 2025 na shule za sekondari kutoka 167 mwaka 2020 hadi 197 mwaka 2025.

Amezitaja baadhi ya shule zilizojengwa kuwa ni Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Simiyu (Simiyu Girls) ya bweni, iliyojengwa kwa gharama shilingi bilioni 4.5. na kuzinduliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 16, 2025. Pia serikali imekamilisha ujenzi wa shule ya amali kwa gharama ya shilingi bilioni 1.6 ambayo nayo ilizinduliwa na Dkt .Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Mkoa unaendelea na ujenzi wa shule ya Sekondari ya Bweni ya Wavulana ya Kanda ya ziwa kwa gharama ya shilingi bilioni 4.1. Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilima 68. Shule hiyo itakapokamilika itakuwa na uwezo kudahili wanafunzi 1,000.

Ameongeza kuwa idadi ya vyumba vya madarasa ya shule za msingi imeongezeka kutoka 4,676 mwaka 2020 hadi 5,802 mwaka 2025 na vyumba vya madarasa ya shule za sekondari kutoka madarasa 1,684 mwaka 2020 hadi madarasa 2,599 mwaka 2025.

"Hatua hii imeongeza uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kutoka 68,177 mwaka 2020 hadi 76,785 mwaka 2025 na wanafunzi walioripoti kidato cha kwanza kutoka 23,376 mwaka 2020 hadi 28,190 mwaka 2025," anasema Anamringi Macha.

## Afya

Katika sekta ya afya Mhe. Macha amesema katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025 mkoa umepokea Jumla ya Shilingi bilioni 26.80 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya afya, shilingi bilioni 10.96 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na shilingi bilioni 31.99 kwa ajili ya ununuzi wa dawa.

Ameongeza kuwa mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya zahanati kutoka 190 mwaka 2020 hadi 242 mwaka 2025, vituo vya afya kutoka 10 mwaka 2020 hadi 21 mwaka 2025 na nyumba za watumishi wa afya kutoka 175 mwaka 2020 hadi 252 mwaka 2025.

Mhe. Anamringi amesema serikali imeimarisha utoaji wa huduma za afya baada ya mkoa kupokea vifaa tiba mbalimbali ambavyo ni CT SCAN, X - Ray za kisasa sita, utrasound machines saba, Viti vya tiba ya meno "dental chair" za kisasa 13, mashine za "X-Ray" sita na mtambo wa kuzalisha hewa tiba ya oksijeni wenye uwezo wa kuzalisha mitungi 80 hadi 100 kwa siku.

Katika sekta ya barabara Mkoa wa Simiyu umepokea jumla ya shilingi bilioni 257.58 katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025 ambapo Shilingi bilioni 70.40 zimetumika kutekeleza miradi ya TARURA na shilingi bilioni 187.19 zimetumika kutekeleza miradi inayosimamiwa na TANROADS.






*Jengo la Huduma za Dharura katika Hospitali ya Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu*



*Daraja la mawe la Mkajagari ambalo limejengwa na Wakala wa Barabara za Vijijini (TARURA) katika Kata ya Mubumba na Bukiriro wilayani Ngara mkoani Kagera.*

Kwa upande wa TARURA barabara za lami zimeongezeka kutoka kilometa 17.8 mwaka 2020 hadi kilometa 27.9 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 52, barabara za changarawe kutoka kilometa 931 mwaka 2020 hadi kufikia kilometa 2,307.85 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 147.8 na barabara za udongo zimepungua kutoka kilometa 3,215.03 mwaka 2020 hadi kufikia kilometa 1,828.78 mwaka 2025 sawa na asilimia 43.

Kwa upande wa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) amesema zimeongezeka kutoka kilometa 102.83 mwaka 2020 hadi kilometa 233.83 Mwaka 2025.

## SGR

Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Shirika Reli Tanzania (TRC) inatekeleza ujenzi wa reli mpya ya kiwango cha ''Standard gauge'' Railways SGR kutoka Dar es salaam mpaka Mwanza kilometa 1,596 na kuendelea na ujenzi wa daraja la ltembe lenye urefu wa meta 150 linalojengwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 8.40 ambapo ujenzi umefikia asilimia 85 kwa sasa.

## Umeme

Kwa upande wa nishati amesema hali ya usambazaji umeme katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025 imeimarika jumla ya shilingi bilioni 130.80 zikiwa zimepokelewa kwa ajili ya kusambaza huduma ya umeme na kati ya hizo shilingi bilioni 127.68 zimetumika kupeleka umeme vijijini na Shilingi bilioni 3.12 zimetumika kupeleka huduma ya umeme mjini.

Mhe. Anamringi amesema mafanikio kadhaa yamepatikana kufuatia uimara wa sekta hiyo ikiwemo huduma ya umeme kufikishwa katika mitaa yote 92 ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi na vijiji 201 vimeshafikiwa na huduma ya umeme hivyo kufikisha idadi ya vijiji vyote 474 kuwa na huduma ya umeme kwa sasa.

## Kilimo

Katika sekta ya kilimo ambayo hutegemewa na wakazi wa Simiyu kwa asilimia 80 kama shughuli kuu ya uchumi, serikali imeimarisha kwa kuongeza vituo vya usambazaji wa mbolea za ruzuku kutokana na kutokuwa na kituo mwaka 2020 hadi kufikia vituo 32 mwaka 2025 hivyo kuchangia matumizi ya mbolea za ruzuku kwa wakulima kutoka tani 277.60 mwaka 2020 hadi tani 805.72 mwaka 2025.

Pia amesema huduma za ugani kwa wakulima zimeimarika na kupitia ajira mkataba za maafisa ugani 409 wa mradi wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) na kuimarisha utoaji huduma za kilimo kidigitali kwa kutoa vishikwambi 173 kwa Maafisa ugani kwa ajili ya kusajili wakulima.

Hali kadhalika amesema juhudi hizo za Serikali zimewezesha ongezeka la uzalishaji wa mazao ya chakula kama mahindi na mpunga kutoka tani 421,451.5 mwaka 2020 hadi tani 1,176,477 mwaka 2025 lakini pia mkoa huo upo katika nafasi ya juu ya uzalishaji wa zao la pamba hai kwa takribani asilimia 60 ya pamba yote inayozalishwa nchini.

## Viwanda na Biashara

Kwa upande wa sekta ya viwanda na biashara amesema kumekuwa na ongezeko la viwanda kutoka 671 mwaka 2020 hadi 1,342 mwaka 2025 kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji na miongoni mwa viwanda hivyo ni viwanda vikubwa kutoka 8 mwaka 2020 hadi 15 mwaka 2025.

## Mifugo

Kuhusu sekta ya mifugo Mhe. Anamringi anasema Mkoa huo ambao ni wa tatu kwa kuwa na mifugo mingi nchini, Serikali imehimiza ufugaji wa kisasa na wenye tija kwa maslahi ya wananchi kupitia utoaji mafunzo, kusambaza madume bora ya ng'ombe aina ya borani 50 yenye jumla ya thamani ya shilingi 125,000,000 na kuwagawia wafugaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa.

## Uvuvi

Katika hatua nyingine amesema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha sekta ya uvuvi kama shughuli zinazofanyika katika mkoa huo kupitia Ziwa Victoria (Busega DC), Ziwa Kitangiri na Ziwa Eyasi (Meatu DC) na miongoni mwa juhudi zilizofanywa ni kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo na vizimba vya samaki ambapo idadi ya vizimba vya kufugia samaki imeongezeka kutoka 21 mwaka 2020 na kufikia vizimba 45 mwaka 2025. Pia serikali inaendelea kutoa mikopo nafuu ya zana za uvuvi.

## Maji

Kwa upande wa sekta ya maji amesema utekelezaji wa miradi ya maji vijijini na mijini katika kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025, umepangiwa jumla ya shilingi bilioni 89.34 kwa ajili ya miundombinu ya kuboresha huduma ya maji na shilingi bilioni 63.73 kati ya hizo zimetumika kutekeleza miradi 85 ya maji vijijini na shilingi bilioni 25.61 zimetumika kutekeleza miradi 61 katika miji ya Bariadi, Maswa, Busega na Meatu ambayo yote imekamilika na inatoa huduma.

Amesema hatua hizo zimeimarisha zaidi hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka asilimia 60.85 mwaka 2020 hadi asilimia 71.0 mwaka 2025 na upande wa mjini umeimarika kutoka asilimia 60.5 mwaka 2020 hadi asilimia 75.7 mwaka 2025.

## Utamaduni

Kwa upande wa Utamaduni, Mhe. Anamringi amesema Mkoa wa Simiyu haujaachwa nyuma kufuatia uwepo wa tamasha maarufu la ngoma linalojulikana kama Mbina ambalo hufanyika kila mwaka wakati wa mavuno kwa kukutanisha vikundi mbalimbali vya ngoma kwa ajili ya kushindana kucheza ngoma. Tamasha hili ni muhimu kwa Mkoa wa Simiyu kwani husaidia kuwaunganisha wananchi wa Mkoa wa Simiyu katika kuendeleza na kuenzi utamaduni.





*Hospitali ya Wilaya ya Karatu, Arusha*

# Arusha Yapaa Kiuchumi, Pato la Wananchi Laongezeka

Na **Mwandishi Wetu - MAELEZO**

Mkoa wa Arusha umepiga hatua kubwa za kimaendeleo katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika kipindi hicho, mkoa wa Arusha ulipatiwa kiasi cha shilingi trilioni 3.5 ambazo zilitumika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye sekta za utawala bora, afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara , nishati ya umeme na utalii.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Kenani Kihongosi, alisema hayo alipozungumza na waandishi wa habari Jijini Dodoma kupitia programu ya 'Tumewasikia, Tumewafikia' iliyoandaliwa na Idara ya Habari - MAELEZO.

Alisema pia kutokana na uwekezaji huo pato la mwananchi katika mkoa huo liliongezeka kutoka shilingi milioni 3.2 mwaka 2020 hadi shilingi milioni 3.6 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Aliongeza kuwa ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo uliongezeka na kufikia asilimia 84.

## Afya

Katika sekta ya afya, Serikali imetoa Shilingi bilioni 94.2 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu. Kiasi hiki kimewezesha ujenzi wa vituo vipya vya afya 87, zahanati 38, na hospitali mpya 8. Kutokana na uwekezaji huo idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeongezeka kutoka 249 hadi 350.

Huduma mpya za kibingwa 11 zimeanzishwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mount Meru, ikiwemo huduma za upasuaji, figo, magonjwa ya ndani, na saratani.

Mhe. Kihongosi alieleza kuwa, Serikali imeimarisha upatikanaji wa dawa kwa kiwango kikubwa kutoka asilimia 65 mwaka 2021 hadi asilimia 93 mwaka 2025, huku ikiongeza mashine za kisasa kama CT-Scan, ECHO na MAMOGRAPHY ambazo zimesimikwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mount Meru.



*Shule ya Sekondari ya Wasichana Arusha*

## Elimu

Katika sekta ya elimu, mkoa wa Arusha ulipatiwa shilingi bilioni 267. Fedha hizi zimetumika kujenga shule mpya 27 za sekondari na 7 za msingi, mabweni 60, maabara 78, na vyoo 940.

Idadi ya wanafunzi wanaonufaika na elimu bila malipo imeongezeka kutoka 390,910 hadi 430,511. Mkoa umeweka mkazo katika elimu maalumu, ambapo shule zinazotoa huduma hii zimeongezeka kutoka 38 hadi 149, na idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu imeongezeka kutoka 1,545 hadi 2,835. Mheshimiwa Kihongosi amebainisha kuwa uwepo wa shule za bweni umewawezesha watoto wa kike, hasa kutoka jamii ya Wamasai, kupata elimu.

## Maji

Katika sekta ya maji, Mkoa wa Arusha umepokea shilingi bilioni 686.9 kati yake shilingi bilioni 568.4 zimetumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (AUWSA) kupanua mtandao wa maji mjini na kuongeza uzalishaji hadi lita milioni 200 kwa siku.

Vijijini, Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilitekeleza miradi 72 yenye thamani ya shilingi bilioni 41.38, na kufanya upatikanaji wa maji vijijini kufikia asilimia 77.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 69.4 mwaka 2020.

## Barabara na Madaraja

Kwa upande wa miundombinu, shilingi bilioni 638.9 zilitolewa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), na kufanya mtandao wa barabara za lami kufikia kilometa 479.88. Pia, Shilingi bilioni 63.3 zilitolewa kwa TARURA kujenga barabara za changarawe na lami, pamoja na kuweka taa za barabarani 495. Mradi mkubwa wa barabara ya Arusha - Kibaya - Kongwa wenye thamani ya shilingi bilioni 221.3 uko mbioni kukamilika.

## Umeme

Kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Umeme Vijijini (REA), Serikali ilitumia shilingi bilioni 117.7 kusambaza umeme katika vijiji vyote 368 vya Mkoa wa Arusha.



## Kilimo na Mifugo

Katika sekta ya kilimo na mifugo, alisema Serikali imetoa shilingi bilioni 86.7 kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa umwagiliaji wa Bonde la Eyasi kwenye eneo la hekta 5,000 ili kunufaisha wakulima 3,000. Kufuatia juhudi hizo uzalishaji wa chakula umeongezeka kutoka tani 450,015 mwaka 2021 hadi tani 536,581 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 19.

## Utalii

Kwa upande wa sekta ya utalii alisema, Mkoa wa Arusha unaendelea kuwa kinara wa shughuli za utalii nchini kutokana na ongezeko la watalii wengi uliochagizwa na Filamu ya Royal Tour iliyochezwa na Mhe.Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.

Alisema mkoa huo ulipokea kiasi cha shilingi bilioni 103 kwa ajili ya uboreshaji wa viwanja vya ndege viwili, uwanja wa Ndege Arusha eneo la Kisongo na uwanja wa ndege ziwa Manyara.

Mhe. Kihongosi alisema, Serikali imetoa kiasi hicho cha fedha kwa lengo la kuboresha viwanja hivyo na kuvipa hadhi ili viweze kuongeza idadi ya abiria na miruko ya ndege kufuatia mkoa wa Arusha kuwa wa pili kitaifa kwa miruko ya ndege na wa tatu kwa idadi ya abiria.

Katika hatua hatua nyingine alieleza kuwa hatua ya Serikali kutoa shilingi bilioni 25 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kisasa la makumbusho ya jiolojia kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itachochea utalii wa kielimu na kiutamaduni mkoani humo.



*Jengo la Makumbusho ya Jiolojia lililopo Karatu, Arusha*

# Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Katika eneo la uwezeshaji wananchi kiuchumi alieleza Serikali kupitia mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wa TASAF imetoa shilingi bilioni 57.22, ambapo shilingi bilioni 38.39 zilitumika kwa kaya maskini. Aidha, aliongeza kuwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyopewa mikopo isiyo na riba viliongezeka kutoka 721 mwaka 2021 hadi 1,380 mwaka 2025.

"Makundi haya yanayoendelea kunufaika na mikopo na kubadili hali zao za kiuchumi. Mathalani, kikundi cha vijana cha USA River kinachojishuhulisha na biashara ya bodaboda kilipokea kiasi cha shilingi milioni 100 kutoka Halmashauri ya Meru na kununua gari aina ya Coster na kikundi cha wanawake wafugaji Halmashauri ya Arusha kilikopeshwa shilingi milioni 35 na kuanzisha mradi wa kutengeneza mikate," alisema Mhe. Kihongosi.

# Michezo

Kwa upande wa Sekta ya Michezo alisema, Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuwekeza kwenye sekta ya michezo ikiwa na lengo la kuimarisha sekta ya utalii, Serikali imetoa Shilingi bilioni 298 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Samia Suluhu AFCON Arusha, ikiwa ni maandalizi ya mashindano ya AFCON mwaka 2027 yanayotarajia kufanyika nchini.





*Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Samia Suluhu AFCON Arusha*




# Mara Wanufaika na Uwekezaji Uliyofanywa na Serikali

Na **Mwandishi wetu – MAELEZO**

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta zote zinazogusa maisha ya wananchi wa mkoa wa Mara hali ambayo imeongeza ustawi na maendeleo ya wananchi, Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Kanali Evans Alfred.

Amesema kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, serikali imetoa shilingi bilioni 43.41 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya kutolea huduma.

Kanali Evans anaeleza kuwa kupitia fedha hizo mkoa wa Mara umetekeleza majukumu mbalimbali yanayolenga kuboresha maisha ya wananchi.

## Afya

Kwa upande wa sekta ya afya, fedha hizo zimetumika kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 321 vilivyokuwepo mwaka 2021 hadi 421 mwaka 2025. Aidha, kliniki za kutolea huduma za afya zimeongezeka kutoka 4 hadi 11, zahanati kutoka 263 hadi 333 na vituo vya afya kutoka 42 hadi 56.

Kwa upande wa hospitali zinazotoa huduma za afya, zimeongezeka kutoka 11 hadi 20, hospitali za halmashauri kutoka tatu hadi 11. Idadi ya nyumba za watumishi imeongezeka kutoka nyumba 221 mwaka 2020 hadi 286 mwaka 2025. Idadi ya watumishi wa afya imeongezeka kutoka 2,515 mwaka 2020 hadi 3,644 mwaka 2025.

Kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya kumepunguza umbali wa wananchi kupata huduma za afya kutoka wastani wa kilometa 15 mwaka 2020 hadi kilometa 5 mwaka 2025. Aidha, maboresho yaliyofanywa na serikali ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kutolea huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere yamepunguza vifo vinavyotokana na uzazi ndani ya mkoa huo.

Kanali Alfred anaeleza kuwa ndani ya mkoa huo huduma za kibingwa zimeanza kutolewa ikiwa ni pamoja na kliniki ya pua, masikio na koo (ENT), Kliniki ya hemophilia, huduma za radiolojia, usafishaji damu, vipimo vya CT scan, wodi inayotoa huduma za watoto njiti (NICU) na huduma za tiba mtandao (Telemedicine).

Aidha, anaeleza kuwa mkoa huo kupitia hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere imeanza kuzalisha gesi tiba ya oksijeni

kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja wanaohitaji huduma ya gesi tiba pamoja na kuhudumia vituo vya afya vya jirani.

Aidha, anaeleza kuwa mkoa huo kupitia hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere imeanza kuzalisha gesi tiba ya oksijeni kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja wanaohitaji huduma ya gesi tiba pamoja na kuhudumia vituo vya afya vya jirani.

Uwepo wa hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere pamoja na uboreshaji mkubwa uliofanywa katika vituo vya kutolea huduma za afya umesaidia kupunguza rufaa za wagonjwa kutoka mkoa wa Mara kwenda Hospitali ya Kanda Bugando kwa asilimia 70.

Kwa upande wa magari ya kubebea wagonjwa mkoa huo umepokea magari mapya ya kubebea wagonjwa 20 na kuongeza idadi ya magari ya kubeba wagonjwa kufikia 39. Aidha, Mkoa wa Mara umepata magari ya shughuli za chanjo tisa na magari mapya 17 kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya ngazi ya mkoa na halmashauri na kufanya magari ya usimamizi kufikia 33.

Pia mkoa huo umepokea pikipiki 75 na kati ya hizo 15 ni za shughuli za utoaji wa chanjo maeneo yasiyo na vituo, 36 ni za ufuatiliaji wa usafi wa mazingira na kuzuia magonjwa ya milipuko na 24 ni za ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za lishe katika Halmashauri zote za Mkoa wa Mara.

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita Mkoa wa Mara umepata bajeti ya dawa na vifaa tiba yenye jumla ya shilingi bilioni 67.92. Bajeti hii imewezesha kuimarisha upatikanaji wa dawa kutoka asilimia 82 mwaka 2020/2021 hadi asilimia 91 mwaka 2024/2025.

## Ardhi

Kwa upande wa sekta ya ardhi, Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutambua uwepo wa changamoto ya migogoro ya ardhi imeweka utaratibu wa halmashauri kupata fedha kwa ajili ya zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Halmashauri za Mji wa Tarime, Wilaya ya Rorya, Manispaa ya Musoma, Mji wa Bunda, Wilaya ya Musoma na Wilaya ya Butiama zimepata jumla ya shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.
.
Mradi huu umewasaidia wananchi kuimarisha usalama wa miliki zao, kupunguza migogoro ya ardhi kutoka 964 mwaka 2020 hadi migogoro 125 mwaka 2025 na kuwawezesha wananchi kupata mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali za kifedha.

Mafanikio mengine ni utoaji wa hati miliki za ardhi umeongezeka kutoka 1,405 mwaka 2020 hadi 5,867 mwaka 2025; utoaji wa hati miliki za kimila umeongezeka kutoka 1,200 mwaka 2020 hadi hati 8,670 mwaka 2025 na vijiji vyenye mpango wa matumizi bora ya ardhi vimeongezeka kutoka 35 mwaka 2020 hadi vijiji 218 mwaka 2025.



# Barabara na Madaraja

Katika eneo la miundombinu ya barabara, Kanali Evans anaeleza kuwa Bajeti ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Mara imeongezeka kutoka shilingi bilioni 6.92 kwa mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 25.71 mwaka wa fedha 2024/2025. Ongezeko hilo limesaidia kufungua barabara mpya, kukarabati barabara za zamani na kuwezesha barabara kupitika misimu yote kwa asilimia 72.7.

Wakala wa Barabara (TANROADS) mkoa wa Mara imetekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara za kimkakati. Barabara hizo ni pamoja Barabara ya Nyamuswa-Bunda-Kisorya-Nansio kipande cha NyamuswaBulamba (kilometa 56.4) kwa gharama ya shilingi bilioni 67.89 ambayo imekamilika.

Barabara ya Makutano ya Juu-Nyamuswa- Ikoma Gate ambayo imejengwa kwa awamu na awamu ya kwanza, kipande cha makutano juu-Sanzate (kilometa 50) kwa gharama ya Shilingi bilioni 60 kimekamilika, awamu ya pili ujenzi wa kipande cha Sanzate- Nata (kilometa 40) kwa gharama ya Shilingi bilioni 39.47 ujenzi wake umefikia asilimia 56.

Pia serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Tarime-Mugumu sehemu ya Mogabiri-Nyamongo (Kilometa 25) kwa gharama ya Shilingi bilioni 34, ujenzi umefikia asilimia 56. Kukamilika kwa miradi hii kutachochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi wa Mkoa wa Mara.

Aidha, mradi wa ukarabati na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma unaendelea kwa jumla ya Shilingi bilioni 35 ambapo umefikia asilimia 58. Kukamilika kwa mradi huo kutachochea ukuaji wa sekta ya utalii katika Mkoa wa Mara. Ujenzi wa mzani wa kupima magari yakiwa kwenye mwendo katika eneo la Rubana, Wilaya ya Bunda umekamilika kwa gharama ya Shilingi bilioni 22.3.

# Elimu

Katika eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa, serikali imezipatia mamlaka hizo zaidi ya shilingi bilioni 85 kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya elimu kwa shule za awali, msingi, sekondari, nyumba za walimu na Vituo vya Walimu (TRC). Jumla ya shule mpya za msingi 20 na sekondari 27 zimejengwa ikiwemo shule ya sekondari ya wasichana ya mkoa wa Mara ambapo mpaka sasa imepokea shilingi bilioni 4.1, ujenzi wa shule ya sekondari ya amali ya mkoa, shilingi bilioni 1.6; na ujenzi wa shule tano za sekondari za amali za halmashauri kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni 2.9.

Katika kuimarisha elimu ya ufundi nchini, Mamlaka ya Vyuo vya Ufundi Tanzania (VETA) imejenga vyuo vitano vya ufundi katika wilaya za Butiama, Rorya, Serengeti, Tarime na Bunda kwa gharama ya shilingi bilioni 12.71.






Ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Butiama umekamilika na mafunzo yameanza kutolewa na vyuo vinne vingine ujenzi unaendelea. Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza fedha za kuwezesha elimu bila malipo kutoka shilingi bilioni 5.6 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 7.5 mwaka wa fedha 2025 kwa shule za msingi; na kutoka Shilingi bilioni 6 hadi Shilingi bilioni 12.85 mwaka 2025 kwa shule za Sekondari. Ongezeko hili limetokana na ongezeko la shule, wanafunzi na maamuzi ya serikali ya kutoa elimu bila malipo kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita.

# Umeme

Katika sekta ya nishati, Mkoa wa Mara umeunganishwa kwenye gridi ya taifa kupitia vituo vya Nyamongo, Musoma, Bunda na Kibara. Hadi kufikia Machi, 2025 mkoa una jumla ya wateja 142,277 na mtandao wa njia za kusambazia umeme msongo wa 33kV kilometa 2,921.83. Aidha, mkoa wa Mara umetekeleza miradi mikubwa tisa kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa gharama ya shilingi bilioni 435.1. Miradi iliyotekelezwa ni ya maboresho ya vituo vya kupooza umeme, maboresho ya mifumo ya usambazaji umeme katika maeneo ya wachimbaji wadogo na maeneo ya wananchi.

Hadi kufikia mwezi Juni, 2025 wilaya zote sita, halmashauri tisa, kata 140, vijiji 458, mitaa 242 na vitongoji 1,555 kati ya 2,502 vina umeme ambayo ni sawa na asilimia 62 ya vitongoji vyote.

# Maji

Katika Sekta ya maji, Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutumia kauli mbiu ya kumtua mama ndoo kichwani imetekeleza miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 426.3 kupitia Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda (BUWSSA), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) na Mamlaka ya Maji ya Mgango - Kiabakari.

Miradi mikubwa ya maji katika Mkoa wa Mara ni pamoja na mradi wa Mgango -Kiabakari-Butiama wenye thamani ya shilingi bilioni 70.5 umekamilika na unatoa huduma kwa wananchi; mradi wa wa Rorya-Tarime wenye thamani ya shilingi bilioni 134.4 ambao umeanza kutekelezwa; mradi wa Mji wa Mugumu, Wilaya ya Serengeti wenye thamani ya Dola za kimarekani 8,755,369 ambao umeanza kutekelezwa.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa upatikanaji wa maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 54 mwaka 2021 hadi asilimia 81 Juni, 2025. Upatikanaji wa maji safi na salama katika miji unaridhisha na hadi kufikia Juni, 2025 upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Musoma ni asilimia 98, mji wa Mugumu asilimia 67, Mji wa Tarime asilimia 77 na Mji wa Bunda ni asilimia 86.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza miradi ya majitaka miwili katika Mkoa wa Mara ambayo inaanzisha mifumo ya majitaka na kuchimba mabwawa ya kusafishia maji taka. Miradi hiyo ni Mradi wa Majitaka wa Manispaa ya Musoma wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 33, ambao unahusisha ujenzi wa mfumo wa maji taka na vyoo katika shule zote za msingi za Manispaa ya Musoma, masoko na maeneo ya wazi. Aidha, mradi wa majitaka wa Butakale katika Mji wa Bunda wenye thamani ya shilingi bilioni 1.728 unaendelea kutekelezwa.



*Muonekano wa mabwawa ya maji taka yanayoendelea kujengwa katika eneo la Makoko Ziwani, Manispaa ya Musoma*

Miradi hii ikikamilika itatoa huduma za majitaka za uhakika katika Manispaa ya Musoma na Mji wa Bunda.

Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza miradi ya ujenzi wa malambo ya kuhifadhia maji ya kunyweshea mifugo katika Wilaya za Bunda na Butiama yenye thamani ya shilingi bilioni 1.46; miradi ya ujenzi wa majosho 11 ya kuogeshea mifugo yenye thamani ya shilingi milioni 308, ujenzi wa kituo cha kukusanyia maziwa katika Kijiji cha Komuge wilayani Rorya kwa jumla ya shilingi milioni 94 mradi huo umekamilika umeanza kazi. Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uhamasishaji wa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika ziwa Viktoria na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025 mkoa ulikuwa na wafugaji wa samaki kwa njia ya vizimba 39 wenye jumla ya vizimba 241.

Aidha, kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) Serikali ya Awamu ya Sita imetoa mikopo kwa wananchi mmoja mmoja na vikundi vinavyojihusisha na ufugaji wa samaki. Hadi tarehe 30 Juni, 2025 mkoa ulikuwa na wanufaika 20 (vizimba 9 na boti 11) waliopata mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.22 katika Wilaya za Rorya, Bunda na Musoma.

## Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Katika kipindi hiki, kuna ongezeko la vikundi vinavyonufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri za Mkoa wa Mara kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutoka vikundi 187 mwezi Novemba, 2020 hadi vikundi 324 Aprili, 2025. Aidha, fedha zinazotolewa kama mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 1.63 Novemba 2020 hadi shilingi bilioni 5.88 mwaka 2025.

Aidha, kumekuwa na ongezeko la vikundi vya wanawake kutoka vikundi 92 Novemba, 2020 hadi 99 Aprili, 2025; vikundi vya vijana kutoka 53 hadi 139 na vikundi vya watu wenye ulemavu kutoka 42 hadi 86. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na vikundi hivi ni pamoja na kuongezeka kwa ajira, uchumi wa vikundi, mtu mmoja mmoja na kupunguza utegemezi wa makundi hayo katika jamii.

Pia Mkoa wa Mara unatekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) ambapo kwa sasa mkoa una jumla ya wanufaika 50,934 hadi kufikia Juni, 2025. Kutokana na mpango huu wananchi kutoka kaya maskini wameweza kuboresha maisha yao kwa kujifunza na kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi.


*Hospitali ya Wilaya ya Singida*

# Miaka Minne ya Rais Samia Singida Yashuhudia Maendeleo Makubwa

Na **Naishooki Makeseni - MAELEZO**

Asilimia 80 ya wakazi wa Mkoa wa Singida hutegemea kilimo na ufugaji kama shughuli kuu za kiuchumi wakizalisha mazao tofauti ya kilimo ikiwemo mtama, uwele na jamii ya mikunde na kwa upande wa ufugaji wananchi wa mkoa huo wanajishugulisha na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku wa asili na nyuki.

Katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita Chini ya Uongozi wa Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan mkoa wa Singida umepata mafanikio makubwa katika sekta zote zinazogusa maisha ya kila siku ya wananchi.

Akizungumza kupitia programu ya Tumewasikia, Tumewafikia inayoratibiwa na Idara ya Habari – MAELEZO, Jijini Dodoma, Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Halima Dendego amesema Serikali ya Awamu ya sita imeupatia mkoa huo jumla ya shilingi trilioni 1.72 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa ustawi wa wananchi.



# Afya

Katika sekta ya afya, Mkoa wa Singida umeshuhudia ongezeko kubwa la vituo vya kutolea huduma za afya, kutoka zahanati hadi hospitali.

Mhe. Dendego anaeleza kuwa vituo vya afya vimeongezeka kutoka 203 mwaka 2020/21 hadi 302 mwaka 2024/25, na zahanati kutoka 173 hadi 246. Aidha, hospitali mpya 5 za wilaya zimejengwa, na majengo mengi ya kutolea huduma za dharura yamekarabatiwa.

Serikali imeimarisha vituo vya magonjwa ya mlipuko na kusimika mitambo 2 ya kuzalisha hewa tiba (Oxygen) katika hospitali ya Wilaya Manyoni na hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mandewa. Upatikanaji wa dawa umeendelea kuimarika kwa asilimia 93, huku utoaji wa chanjo ukivuka lengo la asilimia 100.

# Elimu

Kwenye sekta ya elimu, serikali imejenga shule mpya 142 za ngazi ya msingi, shule mpya 40 za ngazi ya sekondari, na vyuo 4 vya VETA. Elimu bila malipo imepewa kipaumbele kwa kutengewa takribani Shilingi bilioni 48.

# Miundombinu ya Barabara, Madaraja, na Vivuko

Mhe. Dendego anasema sekta ya uchukuzi na miundombinu imeimarika kwa kiasi kikubwa. Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) imeongeza barabara za lami kutoka kilometa 29.8 hadi kilometa 51.1, na barabara za changarawe kutoka kilometa 700 hadi Kilometa 1,892.28. madaraja mapya 17 na makalvati 2,336 pia yamejengwa. Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imejenga kivuko cha chini cha watembea kwa miguu katika baraba



*Daraja la Msingi lililopo wilayani Mkalama Mkoani Singida.*

ra ya Dodoma - Mwanza na daraja la msingi la urefu wa meta 100 katika halmashauri ya Mkalama.

## Maji

Sekta ya maji, ambayo iliwahi kuwa na changamoto, imeimarika sana. Mhe. Dendego anasema upatikanaji wa maji mjini umefikia asilimia 77.6 dhidi ya 53.33 mwaka 2021/22, na vijijini umefikia asilimia 70 dhidi ya 57.9% mwaka 2021/22. Upatikanaji wa maji katika miji midogo kama Manispaa, Ikungi, Iguguno, na Puma umefikia asilimia 86, na ujenzi wa bwawa la maji taka umefikia asilimia 70.

## Kilimo na Ardhi

Katika sekta ya kilimo, ambayo ni tegemeo la wananchi, mkoa umeendelea kujitosheleza kwa chakula, na uzalishaji umeongezeka kutoka tani 649,850 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,325,201 mwaka 2024/2025.

Usajili wa wakulima umeongezeka kutoka 75,398 hadi 293,385, sawa na ongezeko la asilimia 289. Matumizi ya pembejeo za kilimo yameongezeka kwa asilimia 348.4, kutoka tani 1,772.5 hadi tani 7,948.75.

Kuhusu ardhi, Serikali imetatua migogoro 106 na kutoa hati miliki 1,722 za kawaida na 2,345 za kimila.

## Madini

Mapato ya serikali kutoka sekta ya madini yameongezeka kutoka shilingi bilioni 4.8 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 24.2 mwaka 2024/2025. Idadi ya wachimbaji wadogo imeongezeka kutoka 1,091 hadi 1,926. Serikali imejenga masoko 2 ya madini na kuanzisha vituo 4 vya ununuzi.

## Nishati

Kuhusu nishati, amesema matumizi ya mkoa huo yameongezeka kutoka MW 15.19 hadi 21.42 sawa na asilimia 29% kutokana uwepo wa kituo cha kuzalisha na kupozea umeme cha Misuna MW 616 ambacho kimetoa hakikisho zaidi la upatikanaji wa umeme ndani ya mkoa huo na kuchochea ongezeko la shughuli za maendeleo za wananchi. Uimara huo wa upatikanaji wa umeme umeongeza idadi ya watumiaji wa huduma hiyo na idadi ya vitongoji kufikia 1,052 kati ya 2,289.





*Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji katika shamba la Mbegu, Kilimi Nzega Mkoani Tabora*

# Miradi Mikubwa ya Kilimo na Maendeleo Yaboresha Maisha Tabora

Na **Frank MvunglI, MAELEZO**

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mkoa wa Tabora umepata mabadiliko makubwa na chanya, ambayo yamechochewa na maamuzi ya kiongozi mkuu wa nchi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Uongozi wake umeuwezesha mkoa huu, wenye idadi ya watu 3,391,679, kutekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati yenye thamani ya zaidi ya Shilingi trilioni 15 kuanzia Machi, 2021 hadi Juni, 2025. Miradi hii imefanya mageuzi ya kweli na kuboresha maisha ya wananchi katika sekta mbalimbali, ikiwemo kilimo, maji, afya, miundombinu, nishati, na ufugaji.

Akielezea mafanikio haya, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Paul Matiko Chacha, amesisitiza umuhimu wa sekta ya kilimo, ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa mkoa huo.

Mheshimiwa Chacha ameeleza kuwa serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 52.8, kwa ajili ya ruzuku na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji pekee. Kiasi hiki kimetumika kuboresha uzalishaji na kuwafanya wakulima wa Tabora kufanya kilimo chenye uhakika kwa mwaka mzima.
Matokeo ya uwekezaji huu ni Makubwa. Idadi ya skimu za umwagiliaji zimeongezeka kutoka 25 mwaka 2020 hadi 46 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 84. Hii imesababisha eneo la umwagiliaji kupanuka kutoka ekari 16,453.25 mwaka 2020 hadi ekari 37,560.25 mwaka 2025.

Kwa upande mwingine, idadi ya vyama vya ushirika vya umwagiliaji vimeongezeka kutoka 10 mwaka 2020 hadi 23 mwaka 2025, hatua inayoonyesha jinsi wakulima wanavyoungana ili kunufaika na fursa hizi mpya.

# Uboreshaji wa Sekta ya Kilimo na Mifugo

Mbali na umwagiliaji, serikali imeendelea kutoa ruzuku ya mbolea na mbegu ili kuongeza tija. Hali ya upatikanaji wa mbolea imeimarika kwa kiasi kikubwa, kutoka tani 34,109 mwaka 2020/2021 hadi tani 61,504 mwaka 2024/2025.

"Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha mkoa huo kusimamia sekta hii ili kuhakikisha uzalishaji unakuwa wenye tija na usalama wa chakula unaimarika. Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa njia ya ruzuku ya mbolea na mbegu,"anasema Mhe Chacha.

Aidha kutokana na upatikanaji wa mbolea wa uhakika, uzalishaji wa zao la tumbaku umeongezeka kutoka kilo 29,829,742 mwaka 2021 hadi kilo 62,964,460 mwaka 2025.

Katika sekta ya ufugaji, serikali imeendelea kuhamasisha ufugaji wa kisasa. Majosho 16 mapya ya kuogeshea mifugo yamejengwa katika halmashauri zote za mkoa, na hivyo kufanya idadi ya majosho kufikia 95, yenye uwezo wa kuhudumia ng'ombe 889,183.

Huduma za ugani zimeimarishwa, na pikipiki 44, majokofu 6, na vitunza baridi (cool box) 180 vimetolewa kwa ajili ya kampeni za chanjo. Matokeo yake, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 1,200,000 mwaka 2020 hadi lita 2,030,720 mwaka 2025, ongezeko la zaidi ya asilimia 69.

# Afya

Katika sekta ya afya, serikali imetoa shilingi bilioni 34.9 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu. Kiasi hiki kimewezesha ujenzi wa vituo vipya vya afya 30, na kukamilisha maboma 109 ya zahanati.






Mhe. Chacha anaeleza kuwa serikali imetoa fedha za umaliziaji wa maboma ya zahanati 109 pamoja na ujenzi wa nyumba mpya 8 za watumishi na kuongeza miundombinu mipya ya kutolea huduma za Afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Tabora – Kitete, ikiwemo ujenzi wa wodi ya wazazi ya ghorofa 2 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora- Kitete, Ujenzi ambao umefikia asilimia 55% wenye lengo la kupunguza vifo vya Wajawazito na Watoto wachanga ni moja ya mageuzi ya kweli yaliyofanyika katika kipindi hiki.

Sanjari na hayo, Mhe. Chacha amebainisha ongezeko la idadi ya zahanati na Kliniki kutoka 303 mwaka 2020 hadi 378 mwaka 2025 na nyumba za watumishi wa Afya kutoka 291 mwaka 2020 hadi 445 mwaka 2025 ni hatua mojawapo iliyolenga kuleta ustawi kwa wananchi. Mafanikio mengine, katika Sekta ya afya ni kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za Afya kutoka asilimia 75 mwaka 2020 hadi asilimia 91% mwaka 2025. Ongezeko hili limechangiwa na ongezeko la bajeti ya dawa, vifaa na vifaa tiba kutoka Shilingi bilioni 4.23 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi 9.84 kwa mwaka 2024/2025.

## Maji

Kwa upande wa sekta ya maji anaeleza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewatua ndoo kichwani akina mama wa mkoa wa Tabora kwa kuimarisha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi kutoka asilimia 75.7 mwaka 2020 hadi asilimia 89.1 mwaka 2025.

Aidha, jumla ya Shilingi bilioni 147.9 zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji katika mkoa wa Tabora, ambapo kiasi cha shilingi 547.3 milioni ilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya Uviko – 19, Bilioni 1.86 kwa ajili ya miradi ya

"Quick Win" , shilingi milioni 250 kutoka mfuko wa maji, Bilioni 1.62 kutoka Serikali Kuu, 143 Bilioni kutoka mradi wa uendelezaji maji miji 28 na milioni 600 kutoka mfuko wa Maji.

Kasi ya uchimbaji wa visima vya maji imeongezeka kutoka visima 1,024 mwaka 2020 hadi visima 1,118 mwaka 2025, mabwawa ya maji yameongezeka kutoka mabwawa 10 mwaka 2020 hadi mabwawa 13 mwaka 2025 ili kuendana na dhamira ya Serikali kuhakikisha wananchi wake wote wanafikiwa na huduma ya maji safi na salama katika maeneo yao.

Kwa ujumla uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka lita milioni 17.6 hadi lita milioni 39.3 kwa siku, na muda wa upatikanaji wa maji umefikia saa 24 kwa maeneo ya mijini. Vijijini, huduma ya maji safi imeongezeka kutoka asili mia 46 mwaka 2020 hadi asilimia 68.2 mwaka 2025.

# Nishati

Katika sekta ya nishati, serikali imetekeleza miradi yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 353.73. Mafanikio makubwa ni kukamilika kwa uunganishaji wa umeme katika vijiji vyote 722 na vitongoji 1,277 vya Mkoa wa Tabora kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Serikali imewezesha ukamilishwa kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (msongo 132) yenye urefu wa Kilometa 217 (Tabora – Urambo Km 115 na Tabora – Sikonge Km 102) pamoja na vituo vya kupokea, kupoza na kusafirisha umeme vya Uhuru Wilaya ya Urambo (1X35 MVA, 132/33KV) na Ipole Wilaya ya Sikonge (1X15 MVA, 132/33KV).

# Elimu

Kwenye sekta ya elimu, shilingi bilioni 146.69 zimetolewa. Fedha hizi zimewezesha kuongezeka kwa uandikishaji na udahili wa wanafunzi, ufaulu, na kujenga shule mpya katika maeneo yenye uhitaji, hivyo kupunguza umbali wa wanafunzi kwenda shule.

# Miundombinu ya Barabara na Madaraja

Katika sekta ya miundombinu, Mkoa wa Tabora ulipokea shilingi bilioni 225.993. Mtandao wa barabara za lami umeongezeka kutoka kilomita 753.17 mwaka 2020 hadi kilometa 853.4 mwaka 2025. Miradi mikubwa ya kitaifa kama barabara za Usesula – Komanga (Km 108) na Tabora – Nyahua – Chaya (Km 170) imekamilika.a



# Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mikopo ya 10% kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye Ulemavu, kwa mujibu wa Mkuu wa mkoa wa Tabora Mhe. Paulo Chacha imeleta mageuzi makubwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2024/25 jumla ya shilingi bilioni 16.1 zimetolewa na serikali kwa vikundi 1,967, hali inayowawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi.

Uwezeshaji wananchi kiuchumi umesaidia kuimarisha hali ya uchumi ya Mkoa wa Tabora ambapo pato halisi la mkoa limekua kutoka Shilingi trilioni 5.4 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 6.3 mwaka 2024 sawa na ukuaji wa asilimia 17. Vilevile, pato la mtu mmoja mmoja limeongezeka kutoka shilingi milioni 1.77 mwaka 2020 hadi shilingi milioni 1.85 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.5.

# Uwanja wa Ndege

Kwa upande wa usafiri wa anga, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa upanuzi na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora kwa gharama ya shilingi bilioni 24.642, ambapo ujenzi wa jengo la abiria lenye uwezo wa kuchukua wasafiri 120, uzio wenye urefu wa kilometa 6.2, jengo la kuongoza ndege na maegesho ya magari yenye uwezo wa kubeba magari 54 unaendelea.






Air Tanzania



*Hospitali ya Wilaya ya Kyerwa, mkoano Kagera*

# Jinsi Shilingi Trilioni 1.131 Zilivyochagiza Maendeleo Kagera

Na **Jacquiline Mrisho - MAELEZO**

Serikali imeendelea kuboresha maisha na kuinua kipato cha wananchi kiuchumi mkoani Kagera ambapo katika kipindi cha kuanzia mwezi Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025 imeupatia mkoa huo jumla ya Shilingi trilioni 1.131 kwa ajlli ya shughuli za maendeleo.

## Afya

"Katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa, huduma za kibingwa mpya 5 zikiwemo za upasuaji wa pua, koo na masikio, mifupa na magonjwa ya ndani zimeongezwa. Wagonjwa wa rufaa wanaotibiwa ndani ya mkoa wameongezeka hadi kufikia 478,002 ikilinganishwa na wagonjwa 128,305 ambao ni sawa na ongezeko la wagonjwa wa rufaa 349,697 (273%) ambao wangetibiwa nje ya mkoa" anasema Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Hajat Fatma Mwasa.

Mkoa wa Kagera wenye jumla ya wilaya saba, halmashauri nane, tarafa 27, kata 192, vijiji 662, mitaa 66 na vitongoji 3,728 na idadi ya watu 2,989,299 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi 2022 , asilimia 80 ya wakazi wake hutegemea kilimo kukidhi mahitaji yao ya chakula na kiuchumi.

Kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa shughuli za kiuchumi za mkoa huo, serikali imeboresha huduma za afya ili kuhakikisha wananchi wa mkoa huo wanapata huduma bora.

Katika eneo hilo serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 146.34 ambazo ndani ya kipindi cha miaka minne zimeongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya kutoka vituo 249 hadi vituo 336, hospitali kutoka 3 hadi 11, vituo vya afya kutoka 29 hadi 42 na zahanati kutoka 217 hadi 283.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Hajat Fatma Mwassa akiwa msimamizi wa shughuli za serikali ndani ya mkoa huo anaeleza kuwa mapinduzi hayo ya kimaendeleo yamefanyika katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa chachu ya uongozi imara unaoendelea kuleta mabadiliko ya maisha ya Watanzania.



Anaeleza kuwa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umeongezeka kutoka asilimia 85 hadi asilimia 93 ambapo vifaa tiba vya kisasa ikiwemo CT - Scan, ECHO na ECG sasa vinapatikana katika hospitali ya rufaa tofauti na awali ambapo wagonjwa walilazimika kwenda Hospitali za Rufaa ya Kanda Bugando (Mwanza) na Hospitali ya Rufaa ya Taifa Muhimbili (Dar es Salaam).

Vile vile amedokeza kuwa, idadi ya watumishi wa afya imeongezeka kutoka 2,139 hadi 3,542 ambayo ni sawa na ongezeko la watumishi 1,403 (66%) na nyumba za watumishi wa sekta hiyo zimeongezeka kutoka 318 hadi 423 ambalo ni ongezeko la nyumba 105 (33%).

## Elimu

Kwenye sekta ya elimu, serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 128.054 katika mkoa huo ambazo zimeongeza shule za awali na msingi kutoka 942 hadi 1,058, shule za sekondari kutoka 224 hadi 292 zikiwemo shule mpya za amali tatu na shule mpya ya bweni ya wasichana ya Mkoa ya Kagera ambayo imegharimu zaidi ya Shilingi bilioni 4.1, vyuo vya VETA kutoka vinne hadi tisa kikiwemo chuo kipya cha VETA Mkoa cha Burugo kilichogharimu zaidi ya Shilingi bilioni 20.

Aidha, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kampasi ya Kagera unaendelea ambapo kwa sasa umefikia asilimia 70 huku vyumba vya madarasa vya shule za msingi na sekondari vikiongezeka kutoka 9,596 hadi 14,305, ongezeko ambalo limepunguza kiwango cha upungufu kutoka asilimia 50 hadi asilimia 48.9. Nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 2,270 hadi 2,234, maabara za sayansi zimetoka 346 hadi 513 na mabweni kutoka 82 hadi 203.
Pia, jumla ya walimu 1,610 wameajiriwa katika kipindi hicho ambapo walimu wa shule za msingi ni 724 na sekondari ni 886, hivyo kupunguza kiwango cha upungufu wa walimu kutoka asilimia 70 hadi asilimia 57 huku kiwango cha ufaulu kitaaluma kimeendelea kuimarika mkoani humo. Mathalani, ufaulu wa sekondari kutoka asilimia 91.0 hadi asilimia 94.57.

## Maji

Kwa upande wa sekta ya maji serikali imetoa Shilingi bilioni 184.8 kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini. Kwa sasa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama imeongezeka mijini kutoka asilimia 85 hadi asilimia 93 na vijijini kutoka asilimia 76 hadi asilimia 83 huku jumla ya miradi ya maji 41 imetekelezwa (vijijini 23 na Mijini 18) kwa thamani ya shilingi bilioni 164.7.



*Mradi wa Maji Kyaka - Bunazi katika eneo la mlima Katuntu Wilayani Misenyi, Mkoani Kagera.*

Baadhi ya miradi mikubwa iliyotekelezwa katika kipindi hicho vijijini na mijini ni upanuzi wa mradi wa maji Bukoba Mjini uliokamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 3.1, mradi wa maji Kyaka – Bunazi (Missenyi) uliokamilika kwa gharama ya Shilingi bilioni 15. 71, mradi wa maji wa Miji ya Katanga – Omurushaka (Karagwe) umegharimu Shilingi bilioni 64.2 sawa na utekelezaji wa asilimia 64 na mradi wa maji wa Kemondo (Bukoba Vijijini) kwa Shilingi bilioni 4.57 sawa na utekelezaji wa asilimia 100.

## Barabara na Madaraja

Pia,katika eneo la miundombinu ya barabara, serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 117.9 ili kujenga na kuongeza barabara zinazounganisha makao makuu ya mkoa na wilaya kutoka kilometa 783.1 hadi kilometa 800.76, barabara za mijini kutoka kilometa 34.17 hadi kilometa 40.87, barabara za changarawe kutoka kilometa 1,171.54 hadi kilometa 1,275, makalavati kutoka 3,961 hadi 4,535 na idadi ya madaraja kutoka 458 hadi 468.

"Baadhi ya miradi mikubwa ya barabara iliyotekelezwa ndani ya serikali ya awamu hii ni pamoja na; ujenzi uliokamilika wa Daraja la Kitengule lenye upana wa Meta 140 na barabara unganishi Wilaya ya Missenyi na Karagwe za kilometa 18 kwa gharama ya Shilingi bilioni 31.55, ukarabati barabara ya Lusahunga hadi Rusumo kilometa 92 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 153.56 ambao ujenzi wake umefikia 19% na ujenzi wa barabara ya Bugene – Kasulo (BENACO) – Kumunazi kilometa 128.5 kwa gharama ya Shilingi bilioni 92.84 ambao ujenzi wake umefikia 35%," amesema Mhe.Fatma Mwassa.

Ametaja miradi mingine ya barabara kuwa ni upanuzi wa barabara njia nne Rwamishenye - Bandarini (Bukoba) kwa gharama ya shilingi bilioni 5.311 ambao umefikia asilimia 44 pamoja na ujenzi wa madaraja makubwa matano kwa gharama ya shilingi bilioni 45.38 ambapo ujenzi unaendelea.

## Bandari

Aidha, ameeleza kuwa, jumla ya shilingi bilioni 26.241 zimetolewa kwa ajili ya uboreshaji wa Bandari (Bukoba na Kemondo) ambapo utekelezaji bandari ya Kemondo ni sawa na asilimia 100% na Bukoba ni 99%.

## Umeme

Kuhusu nishati ya umeme, serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 103.4 iliyosaidia vijiji vyote 662 kuunganishwa na umeme pamoja na vitongoji 1,763 ambavyo ni sawa na 48% ya vitongoji vyote 3,665.

Miradi minne mikubwa ya kimkakati ya kuzalisha umeme wa maji (HEP) MW 221.8 iliyotekelezwa katika kipindi hiki ni Rusumo/Ngara MW 80 ambao umekamilika, mradi wa Murongo/Kikagati – Kyerwa MW 14 ambao umekamilika, mradi wa Kakono/Missenyi MW 87.8 ambao upo katika hatua ya upembuzi yakinifu na mradi wa Nsongezi/Kyerwa MW 40 ambao upo katika hatua za maandalizi ya awali.

## Kilimo

Katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia sekta ya kilimo, serikali imepunguza tozo katika zao la kahawa kutoka idadi ya tozo 17 hadi 5 pamoja na kuhakikisha kahawa inauzwa katika minada rasmi hali iliyosukuma uzalishaji kuongezeka kutoka tani 53,417 hadi tani 54,203 za maganda kwa mwaka na bei kwa kilo moja kupanda kutoka shilingi 1,200 hadi Shilingi 4,200.

## Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Vile vile kwenye uwezeshaji wananchi kiuchumi, biashara na uwekezaji, vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu vilivyopewa mikopo ya asilimia 10 isiyo na riba vimeongezeka kutoka 630 hadi 1,370 na kiwango cha mikopo iliyotolewa kimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 3.23 hadi shilingi bilioni 9.41. Kaya zilizonufaika kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) zimeongezeka kutoka 36,045 hadi 380,035. Aidha, ruzuku iliyotolewa kwa kaya hizo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 16.82 hadi shilingi bilioni 34.86.

## Vijana

Pia, serikali imewainua vijana kupitia mpango wa mkoa wa kuanzisha mashamba makubwa ya kahawa na migomba ambapo jumla ya vijana 300 wamewezeshwa kuanzisha shamba la kahawa la ekari 300 katika Kijiji cha Makongora, Muleba likiwa ni shamba namba moja na jumla ya vijana 180 wamewezeshwa kujiajiri kupitia kongani 4 za vijana zilizoanzishwa katika Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Kyerwa.

## Biashara na Uwekezaji

Kwa upande wa biashara na uwekezaji, idadi ya biashara rasmi zimeongezeka kutoka 16,376 hadi 25,378 sawa na ongezeko la 55%, wafanyabiashara wadogo (Machinga) waliotambuliwa katika mfumo rasmi wameongezeka kutoka 1,550 hadi 2,821 sawa na 82% na wamewezeshwa kupata ofisi yao iliyogharimu shilingi milioni 35. Aidha, wawekezaji katika mkoa huo wameongezeka kutoka 175 hadi 275, ambapo Kituo cha Uwekezaji (TIC) kimesajili miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 267.16 inayotoa ajira 11,072.

Mkoa huo pia unatekeleza miradi ya kimkakati ya kuchachua uchumi kupitia fedha za mapato ya halmashauri ambapo tangu mwaka wa fedha 2024/25, mkoa umekuwa ukitekeleza miradi ya kimkakati ipatayo 28 inayogharimu jumla ya shilingi bilioni 25.93 ambapo katika bajeti ya mwaka 2024/25 na 2025/26 zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 11.52 ili kuendeleza utekelezaji wa miradi hiyo iliyopo katika hatua mbalimbali.





*Majaji wa Mahakama Kuu wakila kiapo cha Maadili Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma Agosti 29, 2022 Mara baada ya kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

# Katiba na Sheria Waeleza Mafanikio ya Maelekezo ya Dkt. Samia

Na **Grace Semfuko - MAELEZO**

Waziri wa Sheria na Katiba, Dkt. Damas Ndumbaro amesema wizara hiyo imekuwa na mafanikio makubwa hususan katika kipindi cha miaka minne ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani ambapo mojawapo ya mafanikio hayo ni utekelezaji wa kampeni ya msaada wa Kisheria ya Mama Samia ambapo tangu kuzinduliwa kwa kampeni hiyo Aprili, 2023, jumla ya mikoa 25 imefikiwa na kampeni.

Amesema tayari kampeni hiyo imeenea mikoa yote nchini ambapo ili kuhitimisha nchi nzima kwa upande wa Tanzania Bara, Mkoa wa Dar es Salaam kampeni ilitekelezwa Juni, 2025 huku upande wa Zanzibar, utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia umefanyika katika mikoa mitatu na hivyo kukamilisha maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kupitia Kampeni hiyo, jumla ya Halmashauri 180, Kata 1,907 na Vijiji/Mitaa 5,702 ilifikiwa na jumla ya wananchi 2,698,908 walifikiwa na kupata elimu na huduma za kisheria kupitia mikutano ya ana kwa ana. Idadi ya mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria yameongezeka kutoka 84 Novemba, 2021 hadi 377 mwaka 2025. Aidha, idadi ya Wasaidizi wa msaada wa kisheria imeongezeka kutoka 617 mwaka 2021 hadi 2,205 mwaka 2025," anasema Dkt. Ndumbaro.

Amesema, serikali imeanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 184. Aidha, jumla ya watumishi 449 wameajiriwa ili kuwezesha madawati hayo kutekeleza majukumu yake ipasavyo ambapo tangu kuanzishwa kwa madawati hayo, jumla ya wananchi 6,427,738 wamepatiwa elimu juu ya masuala ya kisheria na haki za binadamu.

Aidha amebainisha kuwa, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha uhakiki wa mwisho wa Sheria Kuu 300 kati ya 446 zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni sehemu ya jitahada za Serikali katika kuimarisha utawala bora, utawala wa sheria na kuimarisha misingi ya utoaji haki.

Amesema serikali imeanzisha Kituo cha Huduma kwa Mteja ambapo mwananchi hupata fursa ya kuwasilisha malalamiko na hoja mbalimbali za kisheria moja kwa moja kupitia namba ya simu 0262160360, namba ya Whatsapp 0739101910 na barua pepe kupitia malalamiko@sheria.go.tz.



*Jengo la Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki cha Mahakama ya Tanzania ambacho kilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika eneo la National Capital City Jijini Dodoma.*

"Katika kipindi cha 2021 hadi 2025, idadi ya Majaji imeongezeka kutoka 92 (Mahakama Kuu – 76 na Mahakama ya Rufani - 16) kufikia 146 (Mahakama Kuu – 107 na Mahakama ya Rufani - 39). Pia, idadi ya Mahakimu imeongezeka kutoka 1,412 Aprili, 2021 kufikia Mahakimu 1,426 Aprili, 2025, mashauri yenye umri mrefu Mahakamani ni 2,780 sawa na asilimia 4 ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani. Hivyo, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika zenye mrundikano mdogo wa mashauri Mahakamani.," anasema Dkt. Ndumbaro.

Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki sita umekamilika katika maeneo ya Dodoma, Morogoro, Mwanza, arusha, Kinondoni na Temeke. Aidha, ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki tisa (9) unaendelea katika mikoa mbalimbali, na ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya tatu umekamilika. Aidha, ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya 11 unaendelea.

Dkt. Ndumbaro amesema ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 26 umekamilika na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 72 unaendelea. Ukarabati wa jengo la zamani la Mahakama Kuu Dodoma umefikia asilimia 57. Aidha, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama lililopo Dodoma umekamilika na kuzinduliwa tarehe 05 Aprili, 2025.

Serikali pia imeendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA katika utoaji huduma za kisheria ambapo hadi kufikia Aprili, 2025; asilimia 75 ya mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria imeunganishwa, pia, Wizara imeimarisha matumizi ya mfumo wa Portal ya HAKI SHERIA ambao unatumiwa na wananchi na maafisa Dawati la Msaada wa Kisheria katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 nchini.

Katika kurahisisha tafsiri ya hukumu na kumbukumbu za mashauri, Mahakama imejenga Mfumo wa Kunukuu na Kutafsiri Kumbukumbu za Kimahakama wenye uwezo wa kutafsiri kumbukumbu za kimahakama kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ambapo Mahakama inafanya utaratibu wa kutumia mfumo wa kutafsiri katika Mahakama zote zenye miundombinu ya intaneti nchini.

Ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati na gharama nafuu, serikali imeendelea kufungua ofisi mpya za Mashtaka katika Wilaya ambapo ofisi hizo zimeongezeka kutoka 53 mwaka 2021 hadi 108 mwaka 2025.

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi mwaka 2025, Serikali imesajili jumla ya watoa huduma 123 walioomba kuthibitishwa kama Watoa Huduma za Utatuzi wa Migogoro kwa njia mbadala, hadi Aprili, 2025 wapo Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala 498, kati ya hao, Watoa Huduma za Majadiliano 222, Wapatanishi 174, Wasuluhishi 37 na Waendesha Maridhiano 65.

Serikali kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 watoto 10,824,267 wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Tanzania inazingatia masuala ya haki za binadamu na utawala bora ikiwa ni pamoja na Serikali kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake kikamilifu, Machi 2023, Taasisi inayosimamia Haki za Binadamu Duniani imeipatia Daraja "A" Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi mwaka 2025, sheria mbalimbali zimetungwa na kufanyiwa marekebisho ikiwemo Sheria Kuu 57 na Sheria Ndogo 4,087, pia katika kipindi hicho, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania ilisajili jumla ya wanafunzi 5,333 sawa na asilimia 28 ya wanafunzi 19,025 waliosajiliwa katika miaka 18 tangu kuanzishwa kwa Taasisi.

Aidha, katika kipindi hicho, Taasisi ilitoa wahitimu 2,375 sawa na asilimia 25 ya wahitimu 9,629 waliohitimu tangu kuanzishwa kwa Taasisi mwaka 2008. Hivyo, jumla ya Mawakili 2,375 wameongezeka ambapo pia katika kipindi hicho cha mwaka 2021 hadi mwaka 2025, jumla ya wanafunzi 2,876 wamehitimu mafunzo katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama wakiwemo 1,553 katika ngazi ya cheti na 1,323 katika ngazi ya astashahada.




*Jengo la Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki cha Mahakama ya Tanzania ambacho kilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika eneo la National Capital City Jijini Dodoma.*




*Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato mkoani Geita*

# Geita Yajivunia Samia Kukamilisha Miradi Lukuki

Na **Jacquiline Mrisho - MAELEZO**

Serikali ya Awamu ya Sita kupitia bajeti zake za kila mwaka, imeendelea kuuboresha Mkoa wa Geita kwa kuimarisha sekta mbalimbali zikiwemo za afya, elimu, miundombinu, nishati ya umeme, huduma za maji safi na salama, kilimo, mifugo, madini na uzalishaji.

Kuimarika kwa sekta hizo kumesababisha pato la mkoa na la mwananchi mmoja mmoja kukua. Jumla ya Shilingi bilioni 1.44 zimetolewa katika awamu hii ya sita kwa ajili ya kuboresha sekta hizo.

Vile vile, hali shwari ya ulinzi na usalama katika mkoa inayotokana na ushirikiano wa serikali kupitia vyombo vya dola na wananchi imewezesha kuwapo kwa amani na utulivu.
Maboresho hayo yamefanya hali ya uchumi ya mkoa kuendelea kuimarika huku pato halisi likitoka Shilingi bilioni 7.03 mwaka 2021 hadi Shilingi bilioni 9.12 mwaka 2024 sawa na ukuaji wa asilimia 31. Vilevile, pato la mtu mmoja mmoja limeongezeka kutoka Shilingi milioni 2.7 mwaka 2021 hadi Shilingi milioni 2.8 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 1.6.

## Afya

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa miundombinu ya kutolea huduma za afya, kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi na kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi ambapo mkoa umekamilisha ujenzi wa hospitali za halmashauri za Bukombe, Chato, Geita, Geita Manispaa, Mbogwe na Nyang'hwale na ujenzi wa majengo matatu ya huduma za dharura katika Hospitali ya Bukombe, Katoro na Hospitali ya Halmashauri Nyang'hwale.

Pia mkoa umefanikiwa kukamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Halmashauri ya Geita na ukarabati wa Hospitali ya Halmashauri ya Bukombe na Manispaa ya Geita. Mkoa wa Geita umeongeza idadi ya zahanati kutoka 129 hadi 198, vituo vya afya vimeongezeka kutoka 25 hadi 42, nyumba za watumishi wa afya zimeongezeka kutoka 180 hadi 230, upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka asilimia 80 hadi

asilimia 90, umepunguza vifo vya mama wajawazito kutoka 57 hadi vifo 55 na kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka 5.1% hadi kufikia 4.90%.

# Elimu

Kwa upande wa sekta ya elimu, mafanikio yaliyopatikana yamewezesha kuongezeka kwa uandikishaji na udahili wa wanafunzi, ufaulu pamoja na kupunguza umbali wa wanafunzi kufuata huduma ya elimu.

Aidha mkoa umeweza kuendelea kutekeleza Mpango wa Elimu bila Ada kwa kuongeza fedha za kugharamia mpango huo kutoka Shilingi bilioni 6.48 hadi Shilingi bilioni 19.9 na hivyo kuongeza idadi ya shule za msingi na awali kutoka 641 hadi 792 na idadi ya shule za sekondari kutoka 130 mwaka 2021 hadi 240 mwaka 2025.

Mkoa pia umeongeza idadi ya vyumba vya madarasa ya shule za msingi na sekondari kutoka madarasa 7,206 hadi 10,540, nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari kutoka 2,272 hadi 2,375, ujenzi wa miundombinu ya vyuo vya kati (VETA) kutoka chuo kimoja hadi vyuo 5, vyumba vya maabara kutoka 165 hadi 338.

Aidha, mabweni ya wasichana 74 katika shule za sekondari, mabwalo 19 na hosteli 5, majengo ya utawala 12, matundu ya vyoo 14,133 yamejengwa na kukamilika.

# Maji

Kuhusu sekta ya maji, Serikali ya Awamu ya Sita iliweka kipaumbele cha kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kaya nyingi zaidi zinaunganishwa na huduma ya maji.

Katika kutekeleza azma hiyo, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mkoa huo ni kuimarika kwa huduma ya upatikanaji wa maji safi kwa wananchi kutoka 65% mjini na 61% vijijini hadi asilimia 75% mjini na 65% vijijini, kuongezeka kwa uzalishaji wa maji katika Mji wa Geita kutoka lita milioni 5.2 kwa siku hadi 6.8 kwa siku pamoja na kuongezeka kwa idadi ya vijiji vyenye huduma ya maji kutoka vijiji 204 hadi vijiji 420.



Mkoa umefanikiwa kukamilisha miradi 81 inayotoa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini na kuendelea na utekelezaji wa miradi 20 iliyofikia wastani wa asilimia 51 chini ya usimamizi wa RUWASA, kukamilika kwa miradi 3 ya maji na kuendelea kutekeleza miradi 4 iliyofikia wastani wa asilimia 60 chini ya usimamizi wa GEUWASA pamoja na kuongezeka kwa kasi ya uchimbaji wa visima vya maji kutoka visima 299 mwaka 2021 hadi visima 389 mwaka 2025.

Vilevile, miradi mingine iliyotekelezwa chini ya usimamizi wa GEUWASA ni mradi wa maji Bulera - Nyaseke utakaohudumia wakazi 5,000, mradi wa maji Bung'wangoko utakaohudumia wakazi 6,200, utanuzi wa chujio la maji Nyankanga, ujenzi wa mradi wa maji Mbogwe - Msumbwe utakaohudumia wakazi 7,200, utanuzi wa mtandao wa maji kata ya Mbogwe na Iponya, mradi wa maji katoro - Buseresere na mradi wa maji kutoka ziwa Victoria - Miji 28 utakaohudumia kata 13 za Mji wa Geita na vijiji 19 vya Geita DC.

## Kilimo

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza shughuli za kilimo katika mkoa kwa kuhakikisha kilimo kinakuwa chenye tija na usalama wa chakula unaimarika ambapo jitihada hizo zimesaidia kuanzishwa kwa skimu za umwagiliaji na kufikia skimu 2, kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa mbolea ya ruzuku kutoka tani 1,684.67 hadi tani 5,934.05 na kuimarisha huduma za ugani kwa kununua vitendea kazi ikiwemo pikipiki 153 vipima udongo 5 na vishikwambi 175 kwa ajili ya maafisa ugani.

Mafanikio mengine katika kilimo ni, kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 1,445,814 hadi tani 1,512,761 na mazao ya biashara kutoka tani 67,736 hadi tani 72,820, kuimarisha ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kutoa mafunzo na ujenzi wa vitalu nyumba kutoka vijana 600 hadi vijana 662, kuongezeka kwa vyama vya ushirika kutoka 512 na wanachama 44,375 hadi vyama vya ushirika 600 na wanachama 49,875, kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka tani 9,309 hadi tani 19,632 pamoja na kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi kutoka tani 326,088 mwaka 2021 hadi tani 372,199.

## Ufugaji

Serikali imeendelea kuhimiza ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na utafiti wa mifugo ambapo mkoa umenufaika na usambazaji wa dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo lita 839 na dozi 770,000 za chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng’ombe (CBPP), umekamilisha ujenzi wa majosho 13, umeimarisha huduma za ugani kwa kugawa pikipiki 43 kwa maafisa mifugo na kuanzisha mashamba darasa ya malisho ya mifugo yapatayo hekta 64 sawa na ekari 160.





Pia, serikali imetoa elimu ya ufugaji bora na uboreshaji wa mbari za mifugo kwa kusambaza mbegu bora za mifugo zipatazo 2,000 kwa njia ya uhimilishaji, imeongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita 31,952,400 hadi 35,836,800 na uzalishaji wa nyama kutoka tani 4,626,375 hadi tani 7,710,625.

## Uvuvi

Kwenye uvuvi, mkoa umeimarisha vikundi vya vyama vya ushirika kwa lengo la kupata mitaji na hivyo kuongeza tija katika shughuli za uvuvi ambapo wavuvi wameongezeka kutoka 7,549 hadi 10,001 na idadi ya vyombo vya uvuvi imeongezeka kutoka 997 hadi 2,500. Aidha, idadi ya vizimba vya kufugia samaki imeongezeka kutoka vinne hadi 27 na mitaji iliyotolewa na Serikali kwa wafugaji hao imeongezeka kutoka Shilingi milioni 14 hadi Shilingi 792,563,616.24.

## Madini

Serikali ya Awamu ya Sita inatambua kuwa sekta ya madini ina nafasi ya kipekee katika kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa, upatikanaji wa fedha za kigeni na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Kutokana na hilo, mkoa umefanikiwa kuongeza uzalishaji wa madini kutoka tani 18.21 hadi tani 27.43, kuongeza fedha za kigeni zilizotokana na uuzaji wa madini kutoka dola za Marekani 72,878,325.91 hadi dola za Marekani 92,204,527.35.

Pia, madini yameongeza mapato ya Halmashauri yatokanayo na uchimbaji kutoka shilingi 6,163,170,093.30 hadi shilingi 10,582,192,189.88, mkoa umeongeza masoko ya madini kutoka 10 hadi 20 na utoaji wa leseni kwa wachimbaji wadogo umeongezeka kutoka leseni 903 hadi 9,774.

## Viwanda na Biashara

Mkoa kupitia sekta ya viwanda na biashara, umefanikiwa kuongeza viwanda kutoka 824 hadi viwanda 1,542 na kuongeza ajira za viwandani kutoka 927 hadi 15,161. Pia kuna ongezeko la utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara kutoka leseni 1,346 hadi leseni 2,815.

## Miundombinu ya Barabara na Madaraja

Kuhusu sekta ya miundombinu, mkoa umefanikiwa kuongeza mtandao wa barabara za lami kutoka kilometa 450.86 hadi kilometa 476.87, kuongeza mtandao wa barabara za changarawe kutoka kilometa 1,984.18 hadi kilometa 3,078.48, kukamilisha ujenzi wa madaraja 28 katika Wilaya za Geita, Bukombe,

Chato, Mbogwe na Nyang'hwale na kukamilisha ujenzi wa makalavati 3,444 katika Wilaya za Geita, Bukombe, Chato, Mbogwe na Nyang'hwale.

Mkoa umefanikiwa kukamilisha ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Geita kilichopo Wilaya ya Chato, kukamilisha ujenzi wa madaraja 6 katika wilaya za Geita na Chato na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa TACTIC katika Manispaa ya Geita unaohusu uboreshaji wa barabara ya urefu wa kilometa 17 kwa kiwango cha lami.

## Umeme

Pia, mkoa umeunganisha umeme kutoka vijiji 386 mwaka 2021 hadi vijiji 483 mwaka 2025 na vitongoji 1,021 kati ya vitongoji 2,195 sawa na asilimia 46.5.

Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi ambayo iliunganisha umeme katika vijiji 4 na vitongoji 29 vilivyopo pembezoni mwa njia, umeendelea na utekelezaji wa mkakati wa nishati safi ya kupikia ambapo jumla ya mitungi 16,275 ya gesi iligawiwa kwa mamalishe na umekamilisha mradi wa kusambaza umeme vijijini (REA3R2) ambao ulipeleka umeme katika vijiji 127 na vitongoji 50.

Mafanikio mengine ni kukamilika kwa mradi wa kusambaza umeme katika mitaa na vitongoji 45 vilivyo pembezoni mwa Manispaa ya Geita, kufanikisha maboresho ya miundombinu ya usambazaji umeme katika wilaya zote za mkoa kwa kuondoa nguzo za miti na kuweka za zege ambazo zinadumu kwa muda mrefu zaidi na kujenga njia za kusambaza umeme katika maeneo 52 ya wachimbaji madini wadogo.

## Maliasili na Utalii

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2021 - 2025, mafanikio yaliyopatikana kutokana na sekta ya maliasili na utalii ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi na kuboresha miundombinu ya utalii, kubuni na kuanzisha vivutio vya utalii ikiwemo hifadhi ya Burigi-Chato na kusimamia rasilimali za misitu na nyuki mizinga 426,483.

## Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Katika kufikia azma ya kuleta usawa wa kijamii na kiuchumi kwa wote, serikali imeendelea kuongeza utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na Watu Wenye Ulemavu kutoka Shilingi bilioni 4.9 hadi Shilingi bilioni 8,.6 na kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) ambapo jumla ya Shilingi bilioni 53.2 zilihawilishwa kwa kaya maskini 37,688.



## Michezo na Sanaa

Kwenye michezo na sanaa, mkoa umeboresha miundombinu ya michezo na sanaa kwa lengo la kuimarisha udugu na umoja ambapo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa viwanja vipya viwili vya mpira wa miguu ambavyo utekelezaji wake unaendelea pamoja kuendelea kuhamasisha kuanzishwa kwa vilabu vya michezo (ikiwemo Jogging).

## Miradi ya Kimkakati

Miradi ya kimkakati ya mkoa pia inaendelea kwa lengo la kuongeza mapato na kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi ambapo mkoa umefanikiwa kuendelea na ujenzi wa soko la samaki katika Halmashauri ya Chato, ujenzi wa miundombinu ya stendi ya mabasi Chato kwa gharama ya Shilingi bilioni 14 pamoja na stendi ya Bwanga na kuendelea na ujenzi wa stendi na soko katika Halmashauri ya Bukombe kwa gharama ya shilingi bilioni 16.

Pia, mkoa umekamilisha machinjio ya kisasa katika eneo la mpomvu Manispaa ya Geita, unaendelea na ujenzi wa soko la machinga-Katoro, ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) na ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Magogo katika Manispaa ya Geita wenye uwezo wa kuchukua watazamaji 20,000 kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.1.

## Utawala Bora

Serikali imeimarisha utawala bora ambapo mkoa umefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Mahakama ikiwemo Mahakama za Wilaya ambapo zimeongezeka kutoka 28 hadi 31, vituo vya polisi kutoka 33 hadi vituo 38 na ujenzi wa majengo ya utawala 9, nyumba za viongozi 6 na za watumishi 24 katika Halmashauri za Nyang'hwale, Geita Manispaa, Bukombe, Halmashauri ya Geita, Mbogwe na katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Geita pamoja na Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Nyang'hwale, Bukombe na Mbogwe.

Mkoa wa Geita una Wilaya tano (5), Majimbo ya uchaguzi tisa (9) , Halmashauri sita (6), Miji midogo 2, Tarafa 20, Kata 122, Vijiji 486, Vitongoji 2,195 na Mitaa 65. Wilaya hizo ni Geita, Nyang'hwale, Chato, Bukombe na Mbogwe. Mkoa unajumuisha Halmashauri ya Manispaa ya Geita, Halmashauri za Wilaya za Geita, Nyang'hwale, Chato, Bukombe na Mbogwe. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Geita una wakazi wapatao 2,977,608 ambapo Wanaume ni 1,463,764 na Wanawake ni 1,513,844.





*Bandari ya Tanga*

# Miradi Inayotekelezwa na Serikali Yaboresha Maisha Tanga

Na **Jacquiline Mrisho - MAELEZO**

Miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta za kiuchumi na kijamii mkoani Tanga imeboresha maisha ya wananchi na kupelekea wastani wa pato la mtu mmoja kuongezeka kutoka wastani wa Shilingi milioni 2.7 kwa mwaka 2020 hadi Shilingi milioni 3.4 mwaka 2024 ikiwa ni juu ya wastani wa kitaifa wa shilingi milioni 3.2.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian anaeleza kuwa katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 3.091 ambazo zimetumika kugharamia sekta za afya, elimu, miundombinu, nishati, kilimo, mifugo na uvuvi, uwekezaji, maliasili na utalii.

## Afya

Amesema katika sekta ya afya kumekuwa na ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya, dawa na vifaa tiba ambavyo vimesaidia kuwasogezea wananchi huduma bora za afya karibu na maeneo yao hivyo kupunguza vifo vya wakina mama na watoto kabla, baada na wakati wa kujifungua na kupunguza rufaa zisizo za lazima kwenda nje ya mkoa.

"Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, Mkoa wa Tanga umefanikiwa kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 325 hadi 417. Zahanati zimeongezeka kutoka 287 hadi 361, vituo vya afya kutoka 31 hadi 46, hospitali kutoka 7 hadi 10. Kwa upande wa ununuzi wa dawa na vifaa tiba, mkoa wa Tanga umepokea shilingi bilioni 19.7 za vifaa tiba, ikiwemo CT Scan, Digital X-ray, vitanda vya wagonjwa na magari 12 ya kubebea wagonjwa", anasema Balozi Dkt. Batilda Burian.

Vile vile, mkoa huo umepokea shilingi bilioni 17.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali 6 za wilaya, ukarabati wa hospitali 3, ukarabati na umaliziaji wa hospitali moja katika kila halmashauri za mkoani humo na kupokea shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa majengo 3 ya dharura na shilingi bilioni 1.13 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya.




*Jengo la Mama na Mtoto lililopo Wilaya Korogwe katika Mkoa wa Tanga.*

Mkoa huo pia umepokea shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi katika hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji na vyoo vya watu wenye mahitaji maalumu, miundombinu ya kunawa mikono na vichomea taka katika vituo 71 vya kutolea huduma za afya. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi kufikia Mei, 2025, kuna jumla ya ongezeko la watumishi wapatao 1,195 kati ya waliokuwepo 3,185 hivyo kufikia jumla ya watumishi 4,380 waliopo kwa sasa mkoani Tanga.

## Elimu

Balozi Dkt. Batilda Burian ameeleza mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya elimu kuanzia mwaka 2020 hadi Mei, 2025 kuwa ni kuongezeka kwa fedha za elimu bila malipo kutoka Shilingi bilioni 13.04 hadi Shilingi bilioni 65.9, kuongezeka kwa fedha za uendeshaji wa mitihani kutoka Shilingi bilioni 8.208 hadi Shilingi bilioni 60.3, kuongezeka kwa ufaulu, kuongezeka kwa shule za msingi kutoka shule 1,054 hadi shule 1,148 na shule za sekondari kutoka shule 290 hadi shule 336.

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa nyumba mpya za walimu kwa shule za msingi kutoka nyumba 15 hadi kufikia nyumba 60, kuongezeka kwa ujenzi wa nyumba mpya kwa walimu wa shule za sekondari kutoka nyumba 28 hadi 41 mwaka 2025, kuongezeka kwa mabweni, matundu ya vyoo, kuongezeka kwa maabara 117 katika shule za sekondari, kuongezeka kwa vyuo vya ufundi stadi VETA kutoka chuo kimoja hadi vyuo 7, ujenzi wa miundombinu katika shule 17 za kidato cha 5 na 6 pamoja na ujenzi wa shule mpya ya wasichana ya mkoa iliyopo katika Wilaya ya Kilindi.

## Miundombinu na Madaraja

Kwenye sekta ya miundombinu hasa ujenzi wa barabara, umesaidia kuboresha hali ya uchumi wa wananchi ambapo barabara za kiwango cha lami zimeongezeka kutoka kilometa 124.08 hadi kilometa 165.68, barabara za changarawe zimeongezeka kutoka kilometa 1395.87 hadi kilometa 2,071.38, barabara za udongo zimepungua kutoka kilometa 5,839.2 hadi kilometa 5,136.64.

Aidha, vivuko vya madaraja vimeongezeka kutoka madaraja 91 hadi 100, daraja mfuto kutoka 202 hadi 306, kalavati kutoka 5,019 hadi kalavati 5,398 pamoja na boksi kalavati kutoka 428 hadi boksi kalavati 498.

Utekelezaji wa mradi wa uboreshaji miji (TACTIC) nao umesaidia kuinua uchumi wa wananchi wa mkoa huo ambapo katika Jiji la Tanga zitajengwa kilometa 4 za barabara kwa kiwango cha lami, soko la samaki, soko la makorora, ukarabati wa fukwe raskazone na ujenzi wa mifereji yenye urefu wa kilometa 4, katika Wilaya ya Korogwe zitajengwa kilometa 10.4 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa mifereji yenye urefu wa kilometa 1.9 na Wilaya ya Hande ni zitajengwa kilometa 4.1 kwa kiw-



*Jengo la Huduma za Dharula katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga.*

ango cha lami. Kazi zote za mradi huo ambao upo katika hatua za awali za manunuzi, zipo katika maandalizi huku usanifu ukiendelea kufanywa na Mshauri elekezi kwa Wilaya ya Tanga, Korogwe na Handeni

Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) umesema unaendelea kutekeleza mradi wa ujumuishwaji na ufunguaji fursa za kiuchumi na za kijamii utakaogharimu shilingi bilioni 2.57 ambao unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ambapo jumla ya Kilometa 105.11 zinategemewa kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hizo ni Sindeni-Kwedikwazu kilomita 37.7, Kabuku-Mzundu kilometa 17.6, Michungwani-Bondo-Kwadoya kilometa 18.8,Mkata-Kwasunga ilometa 21 na Kwachaga - Kwankonje kilometa 10.01.

Kwa upande wa mtandao wa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mtandao wake uliongezeka kutoka kilometa 1,528.54 mwaka 2007 hadi kilometa 1,809.30 za sasa ikiwa ni ongezeko la kilometa 280.76.

Aidha, miradi ya barabara mikubwa na ya kitaifa inaendelea kutekelezwa mkoani humo ikihusisha ujenzi wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge)–Saadani–Pangani-Tanga kwa kiwango cha urefu wa kilometa 256, ujenzi wa barabara ya Tanga–Pangani kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 50 sehemu ya kwanza, ujenzi wa daraja la mto Pangani lenye urefu wa meta 525 pamoja na barabara ya maungio yake yenye urefu wa kilometa 14.3, barabara ya mchepuko ya Ushongo yenye urefu wa kilometa 5.9 na barabara za mchepuo za Pangani mjini zenye urefu wa kilometa 5.4 - sehemu ya pili.

Vile vile, Serikali imetekeleza ujenzi wa barabara ya Tungamaa–Mkwaja-Mkange kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 95.2 pamoja na barabara ya mchepuo ya Kipumbwi 3.7 kilometa -sehemu ya tatu (Lot 3), ujenzi wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge)-Mkange Lot 4 na ujenzi wa barabara ya Muheza–Amani kilometa 40 kwa kiwango cha lami.

# Maji

Pia, mkoa umepokea takribani kiasi cha Shilingi trilioni 1.22 kwa ajili ya utekelezaji wa huduma ya maji katika wilaya zote nane za mkoa wa Tanga, fedha hizo zimewezesha kiwango cha upatikanaji maji katika mkoa kuongezeka kutoka 54% hadi 79% na katika maeneo ya vijijini kimeongezeka kutoka 49.7% hadi 75%.

Kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za maji HTM kimeongezeka hadi kufikia 71.9%, Mamlaka ya Maji Mji mdogo wa Songe-Kilindi kufikia 59.6%, Mamlaka ya Maji Mji mdogo wa Lushoto kufikia

68.66% na Mamlaka ya maji Tanga UWASA kufikia 95% hadi Januari, 2024 ambapo idadi ya vijiji vinavyopata huduma ya maji imeongezeka kutoka vijiji 476 mwaka 2020 hadi vijiji 601 mwaka 2025.

Ndani ya kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, jumla ya miradi 151 imetekelezwa kupitia RUWASA ambapo katika miradi hiyo, miradi 96 imekamilika, miradi 65 yenye thamani ya shilingi bilioni 88.5 inaendelea na utekelezaji katika maeneo ya vijijini na mabwawa ya maji mawili yamejengwa na kukamilika (Handeni 1 na Mkinga 1), jumla ya visima virefu 175 vimechimbwa ambapo kati ya visima hivyo visima 63 vimeendelezwa,vituo 1,193 vya kuchotea maji vimejengwa katika maeneo ya vijijini.

Aidha, jumla ya miradi ya maji safi 20 yenye thamani ya shilingi Bilioni 161 inaendelea kutekelezwa chini ya usimamizi wa Tanga UWASA ambapo katika miradi hiyo, miradi 7 imekamilika na wananchi wanapata huduma.

Serikali kupitia UWASA, imewezesha ujenzi wa miundombinu ya uondoshaji majitaka katika miji ya huduma ambapo jumla ya miradi 6 yenye thamani ya shilingi 4.27 inaendelea kujengwa. Aidha, jumla ya visima 108 vimechimbwa na wadau wa maendeleo na kujenga miundombinu ya maji mkoani humo.

## Umeme

Mkoa wa Tanga umepokea shilingi 430,236,577,294.15 kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa umeme mijini na vijijini. Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, idadi ya wananchi wanaotumia umeme imeongezeka kutoka 145,496 hadi 248,213 ikiwa ni ongezeko la 41.4% ambapo jumla ya vijiji 763 sawa na asilimia 100, vimepata huduma ya umeme huku jumla ya vitongoji 2382 vimefikiwa na huduma ya umeme kati ya vitongoji 4531 vya mkoa huo na utekelezaji unaendelea.

## Nishati Safi

Vilevile, mkoa unaendelea kutoa elimu juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi na taasisi za serikali na zisizo za kiserikali. Hadi sasa kuna taasisi 1,493 za serikali zenye watumiaji wa nishati safi.

## Kilimo

Mkoa umepokea shilingi bilioni 33.3 kwa ajili ya shughuli za kilimo zilizowezesha wakulima 11,198 kunufaika na tani



*Tanki la maji safi lililopo Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga.*

4,235.35 za pembejeo kwa gharama ya Shilingi Bilioni 8.1 pia serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 2.5 kuboresha huduma za ugani kwa kusambaza vifaa kama pikipiki 380, vishikwambi 371 na vipima udongo 7. Vile vile mkoa unaendelea na uzalishaji wa mazao mbalimbali ya biashara.

Vilevile, mkoa uliendesha mpango wa Building a Better Tomorrow (BBT) kwa vijana 45 ili kushiriki katika mafunzo ya kilimo cha mazao ya biashara katika Chuo cha Kilimo Mlingano na walishahitimu. Mradi huo uligharimu shilingi milioni 63. Aidha, Bodi ya Korosho Tanzania iliajiri maafisa ugani 22 (internship) kupitia mpango wa BBT kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho.

Mhe. Balozi Dkt. Batilda alinukuliwa akisema "Ili kukifanya kilimo kuwa cha uhakika, serikali inatekeleza miradi mikubwa ya umwagiliaji ikiwemo ujenzi wa bwawa la umwagiliaji Mkomazi kwa shilingi bilioni 18 ambapo upembuzi yakinifu wa Bonde la Mkomazi unafanyika kwa gharama ya shilingi milioni 296 ukarabati wa skimu ya umwagiliaji Mahenge shilingi 2.1 na uchimbaji wa visima kwa wakulima wadogo."

# Mifugo na Uvuvi

Pamoja na kilimo, Mkoa umepokea shilingi bilioni 20.15 kwa ajili ya shughuli za mifugo ikiwemo kujenga majosho 42, kununua boti 14 za uvuvi na kujenga soko la kimataifa la samaki la Kipumbwi ambalo liko hatua za maandalizi ya ujenzi, kuanzisha kituo atamizi kwa vijana 30 kufuga kibiashara kwa kunenepesha ng'ombe 600, kununua boti 50 za unenepeshaji wa viumbe bahari na boti 43 za uvuvi pamoja na kujenga minada 5.

# Viwanda

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi Juni 2025, mkoa umefanikiwa kuongeza idadi ya viwanda vikubwa kutoka 16 hadi 35, vya kati kutoka 23 hadi 69 na vidogo kutoka 2,402 hadi 4,013. Mkoa una ongezeko la ajira takribani 65,275 kufikia Juni, 2025.

# Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mkoa unaendelea na uwezeshaji wananchi kiuchumi ambapo katika kipindi cha mwaka 2020 hadi Juni, 2025, mkoa ulikusanya na kutenga shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya kutoa mikopo ya asilimia kumi kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Katika Mkoa wa



*Boti za Uvuvi pamoja na za kilimo cha Mwani ambazo zilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Pangani mkoani Tanga.*

Tanga, uhawilishaji fedha za TASAF umefanyika kwa awamu 18 na jumla ya fedha kiasi cha shilingi bilioni 26.57 zilipokelewa kwa ajili ya uhawilishaji kwa walengwa, fedha hizo zilipokelewa katika mitaa na vijiji.

## Miradi ya Kimkakati

Kuhusu miradi ya kimkakati, mkoa umeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ili kuwezesha wananchi katika shughuli za kiuchumi ikiwemo uwekezaji wa jengo la kibiashara la Dkt. Samia Suluhu Hassan Bussines Centre, ujenzi wa soko la kisasa la wafanyabiashara wadogo-Machinga, ujenzi wa kituo cha michezo cha Shirikisho la Michezo Tanzania (TFF) ambapo mkoa ulipokea shilingi bilioni 4.51 kwa ajili ya ujenzi huo.

## Miradi ya Kitaifa

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya kitaifa, utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta umekamilika kwa asilimia 53%, mradi wa maboresho ya bandari katika kipindi cha mwaka 2020 hadi Aprili 2025 umefanyika kwa awamu mbili kwa thamani ya shilingi bilioni 429.1. Vile vile, mkoa umepokea shilingi bilioni 1.118 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa kivuko cha MV Tanga ili kusaidia wananchi kupata huduma hiyo kwa urahisi zaidi.

## Utawala Bora

Suala la utawala bora limeendelea kutekelezwa na serikali kwa upana wake ambapo katika kipindi cha mwaka 2020, mkoa ulikuwa na mahakama za mwanzo 65 na wilaya 6 na hadi kufikia mwaka 2025, mkoa una mahakama za mwanzo 67 na wilaya 8. Pia, mkoa umepokea fedha za ujenzi wa majengo ya utawala, samani za ofisi, nyumba za wakurugenzi na wakuu wa Idara.







# Rais Samia: Nguvu ya Michezo Kuunganisha Watanzania

Na **Aron Msigwa - MAELEZO, Dodoma**

Katika miaka minne ya uongozi wake, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara katika kuongeza hamasa ya michezo nchini.

Uwekezaji mkubwa wa serikali na sekta binafsi umewezesha Rais Samia kuunganisha Watanzania wa makundi yote – wazee, vijana, wanawake, wanaume, na watoto – kupitia michezo, hasa mpira wa miguu.

Katika utumishi wake Rais Samia amehakikisha michezo inakuwa chachu ya amani, upendo, na furaha.

## Motisha kwa Wanamichezo na Timu za Taifa

Rais Samia amekuwa akitoa motisha na pongezi kwa timu na wachezaji wanapofanya vizuri. Amekuwa akipongeza vilabu kama Simba na Yanga kwa mafanikio yao katika Ligi Kuu ya NBC na Kombe la Shirikisho la Afrika.

Mnamo Agosti 22, 2021, aliandaa hafla ya chakula cha mchana kwa ajili ya kuwapongeza wanasoka wa Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 23 na wanariadha walioshiriki Olimpiki. Alieleza dhamira ya serikali kukuza michezo kwa kuwa ni afya, ajira, na inakuza hadhi ya Taifa.

Katika kuendeleza hamasa, Rais Samia ameweka historia kwa kutoa ndege kusafirisha wachezaji wa timu mbalimbali. Pia amenunua magoli (Goli la Mama) kwa viwango tofauti, kuanzia Shilingi milioni 1 hadi shilingi milioni 20 kwa timu zinazoshiriki michuano ya kimataifa, ikiwemo timu za Simba, Yanga, Azam, na timu za Taifa za wanaume na wanawake. Mfano wa hivi karibuni ni ndege aliyotoa kwa timu ya Taifa (Taifa Stars) kwenda Morocco kwa ajili ya mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia, pamoja na motisha ya shilingi milioni 500 kwa kufuzu AFCON 2023.




# Uwekezaji katika Miundombinu ya Michezo

Serikali imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo na kuondoa kodi kwenye nyasi bandia ili kuongeza hamasa ya michezo. Kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ujenzi wa Akademia ya Michezo unaendelea katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya-Mwanza.

Pia, ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Benjamin Mkapa umekamilika kwa Shilingi bilioni 31, ikiwa ni maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027. Ukarabati huo ulihusu vyumba vya wachezaji, waamuzi, mifumo ya taa, eneo la VIP, na ubadilishaji wa viti vyote. Maeneo mengine yaliyoboreshwa ni mifumo ya matangazo, TEHAMA, nyasi za uwanja, na mifumo ya viyoyozi, umeme, na maji.



*Uwanja wa Benjamin Mkapa baada ya kufanyiwa ukarabati.*



## Mafanikio ya Timu za Taifa na Vilabu

Chini ya uongozi wa Rais Samia, kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30, timu sita za Taifa zimeweza kufuzu katika mashindano makubwa. Tanzania imefuzu Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) kama mwenyeji, na Taifa Stars ilishiriki michuano ya AFCON nchini Ivory Coast. Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) ilishiriki mashindano ya WAFCON, na Timu ya Taifa ya Futsal ya Wanawake imefanikiwa kufuzu Kombe la Dunia 2025.

Kwa upande wa vilabu, Tanzania imefanikiwa kupeleka timu nne—Yanga, Simba, Singida Fountain Gate FC, na Azam FC—katika mashindano ya Kombe la Shirikisho na Klabu Bingwa Afrika.

Ligi Kuu ya NBC imeendelea kuimarika na sasa inatajwa kuwa miongoni mwa Ligi 5 bora Barani Afrika.

Maeneo mengine ambayo Rais Samia ametoa motisha ni Kombe la CRDB, Michuano ya CHAN na michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyomalizika hivi karibuni.

Tanzania pia ilikuwa mwenyeji wa uzinduzi wa mashindano ya African Football League (AFL) Oktoba 20, 2023.

Rais Samia kwa kufanya hivyo amekuwa akisisitiza kuwa kama Taifa tunahitaji kuwa na mafanikio katika sekta hiyo ndiyo maana serikali imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo chini ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanaendelea kuwa na furaha.

## Mafanikio katika Michezo Mingine

Riadha: Wanariadha wa Tanzania wamefanya vizuri kimataifa. Magdalena Shauri alishinda medali ya shaba kwenye mbio za Marathon za Berlin. Alphonce Simbu alishika nafasi ya pili kwenye mbio za Shanghai.

Aidha, mwaka 2024 wanariadha kutoka Tanzania, Alphonce Simbu, Jackline Sakilu na Magdalena Shauri walishiriki katika mashindano ya Olimpiki yaliyofanyika, Paris nchini Ufaransa.

Gofu: Timu ya Taifa ya Gofu ya Wanawake ilikuwa mshindi wa kwanza wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika Rwanda.

Kuogelea: Timu ya Taifa ya kuogelea ilishika nafasi ya pili kwenye mashindano ya "CANA Zone 3" nchini Rwanda.

Mabondia wa Tanzania wameendeleza ubabe kwa kushinda medali mbalimbali. Yusuf Changalawe alishinda medali ya Fedha katika mashindano ya kufuzu Olimpiki nchini Senegal.

# Mchango wa Sanaa na Kiuchumi

Maboresho yaliyofanywa na serikali yameongeza kiasi cha mirabaha iliyogawiwa kwa wasanii waliosajiliwa COSOTA kutoka shilingi milioni 245 hadi shilingi milioni 687.7. Hii imewezesha wasanii kunufaika na kazi zao. Vibali vya wasanii wa ndani kwenda nje ya nchi vimeongezeka kutoka 122 hadi 1,492, na vibali vya wasanii wa nje kuja nchini vimeongezeka kutoka 75 hadi 623.

Sekta hii ya michezo imeendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo ya nchi kupitia ajira, ukuaji wa mapato, na uchochezi wa sekta zingine za kiuchumi kama utalii, usafirishaji, na biashara. Uongozi wa Rais Samia unaendelea kuacha alama isiyofutika katika maendeleo ya michezo nchini.

Rais Samia Suluhu Hassan amekua kiongozi mwonesha njia na mchezaji mahiri nje ya uwanja. Katika hili ameiwezesha Tanzania ieendelee kufanya vizuri, kupata umaarufu na kuimarisha uhusiano wa Kidiplomasia na mataifa mbalimbali kupitia michezo.

Katika kuhakikisha Watanzania wanaendelea kupata mafanikio kwenye michezo, serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeendelea kusimamia maandalizi ya michuano ya AFCON 2027 kuhakikisha yanakwenda vizuri ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo katika mikoa ya Dar es salaam, Dodoma na Arusha.



*Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi akikabidhi kiasi cha Shilingi milioni 20 kwa Timu ya Taifa Stars baada ya ushindi wa goli 2 - 0 dhidi ya Burkina Faso katika Mashindano ya CHAN Agost 2, 2025..*





*Katibu Mkuu wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa akizungumza na Timu ya Taifa Stars baada ya ushindi wa goli 2 - 0 dhidi ya Burkina Faso katika Mashindano ya CHAN Agost 2, 2025.*





*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na washindi mbalimbali wa Tuzo za Komedi mara baada ya hafla ya utoaji wa Tuzo hizo katika ukumbi wa The Super Dome, Masaki Jijini Dar es Salaam Februari 22, 2025.*




# Alphonce Simbu Atwaa Medali ya Dhahabu Mashindano ya Riadha Duniani 2025

Na **Mwandishi Wetu**

Miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta za kiuchumi na kijamii mkoani Tanga imeboresha maisha ya wananchi na kupelekea wastani wa pato la mtu mmoja kuongezeka kutoka wastani wa Shilingi milioni 2.7 kwa mwaka 2020 hadi Shilingi milioni 3.4 mwaka 2024 ikiwa ni juu ya wastani wa kitaifa wa shilingi milioni 3.2.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian anaeleza kuwa katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 3.091 ambazo zimetumika kugharamia sekta za afya, elimu, miundombinu, nishati, kilimo, mifugo na uvuvi, uwekezaji, maliasili na utalii.
Amesema katika sekta ya afya kumekuwa na ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya, dawa na vifaa tiba ambavyo vimesaidia kuwasogezea wananchi huduma bora za afya karibu na maeneo yao hivyo kupunguza vifo vya wakina mama na watoto kabla, baada na wakati wa kujifungua na kupunguza rufaa zisizo za lazima kwenda nje ya mkoa.

"Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, Mkoa wa Tanga umefanikiwa kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 325 hadi 417. Zahanati zimeongezeka kutoka 287 hadi 361, vituo vya afya kutoka 31 hadi 46, hospitali kutoka 7 hadi 10. Kwa upande wa ununuzi wa dawa na vifaa tiba, mkoa wa Tanga umepokea shilingi bilioni 19.7 za vifaa tiba, ikiwemo CT Scan, Digital X-ray, vitanda vya wagonjwa na magari 12 ya kubebea wagonjwa", anasema Balozi Dkt. Batilda Burian.

Vile vile, mkoa huo umepokea shilingi bilioni 17.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali 6 za wilaya, ukarabati wa hospitali 3, ukarabati na umaliziaji wa hospitali moja katika kila halmashauri za mkoani humo na kupokea shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa majengo 3 ya dharura na shilingi bilioni 1.13 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya.


TANZANIA
TDK
ATHLETICS
CHAMPIONSHIPS


TANZANIA
TDK
WORLD ATHLETICS CHAMPIONSHIPS TOKYO 25
WORLD ATHLETICS CHAMPIONSHIPS TOKYO 25
Tokyo


TBS
TDK
WGV
ITALIA
WORLD ATHLETICS CHAMPIONSHIPS TOKYO 25



Idara ya Habari MAELEZO
S.L. P 25
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 2322129
Barua pepe: maelezo@michezo.go.tz
www.maelezo.go.tz

@MsemajiMkuuwaSerikali
@MaelezoNews